*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo




| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00056 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumanne Machi 19 - 26, 2024 |

# Ni miaka 3 ya kishindo

- Miradi mikubwa inaendelea
- Pesa zimeshushwa hadi vijijini
- Tunaridhiana, tunavumiliana



# DUWASA inavyopambana kukidhi huduma za maji Dodoma

- Asilimia 91 ya wakazi wanapata maji safi na salama
- Mkakati wa sasa ni kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria





**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), ina jukumu la msingi la kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka kwa wakazi wa Jiji la Dodoma, miji ya Chamwino, Kongwa, Bahi na Kibaigwa. Mamlaka inaendelea kutekeleza mipango mbalimbali katika kutimiza lengo hilo la msingi, ambapo ipo mipango mbalimbali inayotekelezwa kutatua changamoto hizo.

### HALI YA UPATIKANAJI MAJI

Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, amesema kwa sasa, Jiji la Dodoma lina wakazi 765,179 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ambapo takriban asilimia 91 wanapata huduma ya majisafi na salama kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na migao. Joseph anasema tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonesha kuwa, mahitaji ya maji kwa Jiji la Dodoma ni lita milioni 149.5 kwa siku. Aidha, hadi kufikia mwaka 2051, tathmini inaonesha kwamba mahitaji halisi ya maji yataongezeka na kufikia lita milioni 417.3 kwa siku.

Mkurugenzi Mtendaji Joseph anafafanua kuwa chanzo kikuu cha maji kwa matumizi ya wakazi wa Jiji la Dodoma, ni visima virefu vilivyochimbwa katika bonde la Makutupora eneo la Mzakwe.

"Miundombinu ya uzalishaji na uwezo wa usafirishaji maji, ni lita milioni 61.5 kwa siku. Aidha, kuna vyanzo vingine vidogo kwa maeneo mahsusi ya Ihumwa kwa ajili ya Mji wa Serikali, Iyumbu kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Kata ya Iyumbu, Hospitali ya Benjamin Mkapa na Kata ya Nghong'onha, ambavyo kwa pamoja, vinazalisha lita milioni 5.6 kwa siku," anafafanua.

Anaongeza kuwa chanzo kipya cha Nzuguni kilichozinduliwa hivi karibuni, kina uwezo wa uzalishaji wa lita milioni 10.3 kwa siku. Vyanzo vyote hivyo na vingine vidogo vidogo, vinafanya uzalishaji kuwa jumla ya lita milioni 79.12 kwa siku, wakati mahitaji ya sasa ni lita milioni 149.5 kwa siku. Mhandisi Joseph anasema kwa sasa upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma ni lita milioni 70.38 kwa siku na kwamba upungufu huu unaongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi na kijamii katika Jiji la Dodoma.

### UTEKELEZAJI WA MIRADI

Mhandisi Joseph anasema ili kuhakikisha Dodoma inakuwa na maji ya uhakika katika mipango ya muda mrefu, serikali imepanga kuanza kutekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Anasema mradi huo utahusisha ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, matangi, vituo vya kusukuma maji na mabomba ya kusafirisha maji kutoka Mwanza hadi Dodoma.

"Wizara ya Maji imeshatangaza zabuni ya Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu, zabuni za mkandarasi wa ujenzi na kusimamia utekelezaji wa mradi huu. Wizara imewasilisha mkataba wa kazi hii kwa Mwanasheria Mkuu kwa uchunguzi," anasema.

Anasema serikali imetoa fedha za kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa la Farkwa ili kutosheleza mahitaji ya maji jijini Dodoma na maeneo ya pembezoni hadi mwaka 2038. Mhadisi Joseph anasema bwawa la Farkwa litajengwa katika Kijiji cha Mombose Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma ambapo utahusisha ujenzi wa bwawa, chujio, matangi ya kupokelea maji na ujenzi wa bomba kuu kutoka Farkwa hadi Dodoma linalokadiriwa kuwa na urefu wa kilomita 117 litakalogawa maji kwa vijiji vyote vilivyopo ndani ya umbali wa kilomita 12 pande zote za bomba hilo katika Wilaya za Chemba, Chamwino, Bahi na Dodoma.

"Mradi utahusisha pia na utunzaji na uhifadhi wa chanzo na unakadiriwa kugharimu takribani Dola za Marekani milioni 135.8 (sawa na Sh. bilioni 312.08) katika awamu ya kwanza. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), imeshatenga fedha hizo kutekeleza awamu hii." Anasema.

Anasema hatua iliyofikiwa hadi sasa Mshauri kampuni ya SU-YAPI Engineering and Construction Inc, JV Dar Al – Handasah and Don Consult Ltd, anaendelea na usanifu kwa muda wa miezi sita tangu Oktoba, mwaka jana. Mradi utafanyika kwa awamu tatu mpaka kukamilika kwake.

Katika hatua nyingine, anabainisha kuwa DUWASA inaendelea kutekeleza mradi wa maji safi Nzuguni lengo ni kuboresha huduma ya usambazaji maji katika kata na jiji la Dodoma kwa ujumla, kwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita 68,600,000 hadi 76,000,000 kwa siku, sawa na ongezeko la asilimia 11.7.

Anafafanua kuwa hadi sasa mradi umefikia asilimia 99 DUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi huu kwa kutumia wazabuni saba ambao ni TANESCO, Tanelec Limited Arusha, Master Drilling and Exploration Ltd, Help Desk Ltd, Davis Shitriff Ltd, Judex Contractors na Tanzania Steel Pipes.

Anasdema mradi huo umehusisha uchimbaji na uendelezaji wa visima vinne, ununuzi wa transfoma sita, ujenzi wa mtandao wa kusafirisha na kusambaza maji wenye takriban kilomita saba, ujenzi wa matangi mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 3,500,000 na ujezi wa vibanda vya kuendeshea pampu.

"Mradi huu mpaka kukamilika kwake utagharimu Sh. bilioni 4.3. Fedha zote za kutekeleza mradi huu, zinatolewa na serikali kupitia mapato yake ya ndani katika kuhakikisha hali ya huduma ya maji inaimarika jijini Dodoma.

DUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, inachimba visima vingine vitano na kisima kimoja kikubwa chenye kina cha mita 300 katika eneo la Nzuguni, anasema Mhandisi Joseph.

"Mkandarasi Kampuni ya PNR Ltd, ameanza kazi ya uchimbaji wa visima vitano kwa gharama ya Sh.milioni 220 eneo la Nzuguni na Mkandarasi kampuni ya Shanxi Constrtuction, anachimba kisimakirefu chenye kina cha mita 300 chini ya ardhi eneo la Nzuguni kwa gharama ya Sh. milioni 570," anaeleza.

"DUWASA inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuipa kipaumbele kutatua changamoto za upatikanaji wa maji na uondoshaji majitaka katika Jiji la Dodoma na miji ya Bahi, Chamwino, Kongwa na Kibaigwa.

### WANANCHI WANENA

Wakizungumza jijini hapa kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma wamesema kutokana na ongezeko la idadi ya watu, upo umuhimu kwa serikali kuweka mikakati madhubuti yakuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji.

Mkazi wa Kata ya Makulu, Samuel Mbenjile, anasema suala la mgao wa maji limekuwa ni changamoto katika baadhi ya maeneo kwani baadhi ya siku hayatokei, lakini mwisho wa mwezi bili zinatolewa.

Anasema Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali, idadi ya watu inaongezeka kila siku, lakini vyanzo vyamaji ni Vilevile.

"Tunaomba serikali ichukue hatua za haraka ili kunusuru wananchi. Ongezeko la idadi ya watu, shughuliza kijamii, kiuchumi zinazotumika maji, uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji pamoja na matumizi ya teknolojia yenye gharama kubwa, ni miongoni mwa sababu zinazoathiri huduma ya maji maeneo yamijini," anasema.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Jenipher Simon, anasema serikali kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi, inapaswa kuelekeza nguvu na rasilimali fedha katika usimamizi wa sheria, kanuni na sera ya kutunza, kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji vilivyopo.

Anasema suala la kupanda, kutunza na kuhifadhi miti, liwe ajenda ya kudumu ya kitaifa kwa kilaMtanzania kuhimizwa kupanda miti katika eneo lake.

"Haikubaliki kuona Watanzania wanakosa huduma ya uhakika ya maji safi na salama licha ya Taifa kujaliwa rasilimali nyingi ya maji, ikiwemo mito inayotiririsha maji kipindi chote cha mwaka, Maziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika na mvua zinazonyesha hadi mara mbili kwa mwaka," anasema.

DUWASA imetekeleza jumla ya miradi 26 ya kuboresha hali ya huduma ya maji katika Jiji la Dodoma na miji ya Bahi, Chamwino, Kongwa na Kibaigwa ambayo imegharimu Sh. 28,709,093.67.

DUWASA inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuipa kipaumbele katika kutatua changamoto za upatikanaji wa maji na uondoshaji majitaka jijini Dodoma na miji ya Bahi, Chamwino, Kongwa na Kibaigwa.

# Huyu ndiye Samia, mkali katika matumizi ya fedha za umma

**Na Mwandishi Wetu**



UKIMWANGALIA, utaamini kuwa ni mpole, mwenye huruma na asiyependa makuu, lakini linapokuja suala la fedha za umma, sura yake hubadilika na kuwa mkali kuliko hata ulivyotarajia. Huyu si mwingine bali ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan

"Kwa wale wanaotaka kuzijua rangi zangu halisi, wajaribu kudokoa fedha hizi au wabadilishe matumizi yale bila maelewano. Kila kona ya nchi inakwenda kuwa na ujenzi wa miradi ya maendeleo. Kwenye fedha hii, sina huruma na mtu."

Hii ni kauli ya Rais Dk. Samia aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Serikali wa kuinua uchumi kwa kutumia fedha za mkopo wa Sh. trioni 1.3 uliotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na kukabiliana na ugonjwa virusi vya corona.

Rais Dk. Samia alitoa kauli hiyo kali kwa watendaji huku akiwaelekeza kuondoa urasimu, kudhibiti mianya ya rushwa na ufanisi wa miradi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na serikali, vipaumbele mbalimbali vilivyopangwa kufanyika kutokana na fedha za mkopo huo.

Baadhi ya maeneo ambayo yalilengwa zaidi ni kama ifuatavyo;-

- Ununuzi magari ya wagonjwa ya kisasa 20 na magari ya kawaida 365.
- Ujenzi wa vituo vya dharura na vifaa kwa hospitali zote kuanzia Taifa hadi halmashauri.
- Uimarishwaji wa mfumo wa usambazaji na ununuzi wa mitungi ya gesi katika hospitali za rufaa.
- Usimikaji wa vinu 44 vya hewa ya Oksijeni kwa ajili hospitali za Taifa na halmashauri
- Ununuzi wa mashine za X-Ray 85
- Ufungaji wa mashine za MRI kwa hospitali za Taifa, kanda na mikoa
- Ujenzi wa vituo vinne vya Telemedicine.
- Ujenzi wa vyumba na ununuzi wa vifaa vya uangalizi maalum (ICU) 72 kwa ngazi ya Taifa, kanda, mikoa na baadhi ya halmashauri.
- Utekelezaji wa miradi ya maji kwa wananchi.
- Utekelezaji miradi ya elimu kama vile madawati, vyumba vya madarasa katika vyuo 17.
- Vituo vinne vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ni dhahiri kwamba Rais Dk. Samia amekuwa akikerwa na ripoti za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambazo zimekuwa zikiibua ubadhirifu, upotevu wa fedha na matumizi yasiyoeleweka ndani ya taasisi za serikali.

Akizungumza jijini Dodoma wakati wa kuzindua Kampeni ya Maendeleo dhidi ya UVIKO-19, Rais Dk. Samia aliagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kutoa vibali vya utekelezaji wa miradi kwa kupata mzabuni mwenye uwezo wa kutekeleza mradi badala ya kuitisha zabuni kwa mfumo wa ushindani wa wazabuni wengi, ambayo kwa mujibu wa sheria za nchi, huchukua takriban miezi mitatu au zaidi hadi kutangazwa mshindi.

"Kwa wasimamizi, hii miradi iishe kwa miezi tisa. Sitaki tusiitekeleze kwa vizingizio. Wazabuni wapatikane kwa single sourcing, mkitaka kufanya kwa utaratibu mwingine wa kutangaza zabuni kwa miezi mitatu, mtatuchelewesha. Twende na single sourcing. Halmashauri, idhini itolewe na PPRA pia urasimu uondolewe katika misamaha ya kodi kwa vifaa kutoka nje ya nchi vinavyokuja kutumika katika miradi hiyo na CAG nawe fuatilia kwa karibu fedha za miradi hii," alisisitiza Rais Dk. Samia.

Karibu kila mwaka, ripoti za CAG imekuwa ikiibua ubadhirifu, uvunjaji wa sheria, miradi hewa na mianya ya ulaji rushwa.



# Ni miaka mitatu ya

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amewatumikia Watanzania kwa kishindo katika kuhakikisha fedha za maendeleo zinafika sekta zote kuanzia ngazi ya Taifa hadi vijijini.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amethibitisha hayo hivi karibuni kuwa Rais Dk. Samia amefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali katika kila sekta za maendeleo kwa muda mfupi, nguvu na kasi kubwa.

Anasema Rais Dk. Samia anatekeleza miradi mbalimbali ya maeneo katika sekta zote za maendeleo kuanzia ngazi ya Taifa hadi vijijini ili kuhakikisha maisha ya Watanzania yanakuwa bora.

Aidha kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia kama kiongozi wa nchi, imekuwa ya kiutendaji zaidi huku akitatua changamoto nyingi kama tatizo la umeme, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), miundombinu ya barabara, maji, usafirishaji, mawasiliano, elimu, kilimo, uvuvi, madini, afya na kadhalika.

Licha ya ujenzi na ukarabati wa miradi mbalimbali katika kipindi hicho, Rais Dk. Samia, ameonyesha utawala unaojali maslahi ya watu ili kujenga ustahimilivu kwa kuepuka migongano, kutafuta suluhu na mapatano pale kunapotokea kutoelewana.

Pia ameleta mageuzi yatakayochochea kukua na kushamiri kwa nchi pamoja na kujenga na kuimarisha mifumo mbalimbali katika nchi na kuimaisha demokrasia.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, amesema uongozi wa Rais Dk. Samia umeimarisha utawala unaojali maslahi ya watu ili kujenga ustahimilivu kwa kuepuka migongano, kutafuta suluhu na mapatano pale kunapotokea kutoelewana, kuleta mageuzi yatakayochochea kukua na kushamiri kwa nchi pamoja na kujenga na kuimarisha mifumo mbalimbali katika nchi.

Alitoa nasaha hizo wakati wa Kongamano la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), kuelekea miaka mitatu ya Rais Dk. Samia na miaka 47 ya kuzaliwa kwa CCM lililofanyika mkoani Kigoma, Januari 29, mwaka huu.

Katika hatua nyingine kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, Rais Dk. Samia ameiwezesha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Tanzania (DCEA), ambayo imefanikiwa kukamata jumla ya kilogramu 3,182 za dawa za kulevya aina ya Heroin na Methamphemine zikiwa kwenye vifungashio vya kahawa na majani ya chai.

Dawa hizo zimekamatwa katika operesheni maalum iliyofanyika jijini Dar es Salaam na Iringa kati ya Desemba 5 hadi 23, 2023.

Kamishna Jenerali Aretas Lyimo amesema, tangu udhibiti uanze DCEA hazijawahi kukamata kiasi kikubwa cha dawa kama ilivyo sasa na iwapo zingefanikiwa kuingia sokoni watu milioni 76.3 wangeathirika.

Jenipher Kanumba anasema miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani amefanya kazi kubwa, kwa mfano, katika miradi ya mageuzi miradi ya maji zaidi ya 1,000.

Baadhi ya miradi ambayo Rais Dk. Samia amefanikiwa kutekeleza katika kipindi kifupni ni kama ifuatavyo;

**SEKTA YA MAJI:**


Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu Zuhura Yunus anasema, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia hali ya upatikanaji wa huduma ya maji







**Hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeimarika kutoka wastani wa asilimia 70.1 hadi 77 na mijini asilimia 84 hadi 88 imeimarika kutoka 2020 mpaka Desemba 2022.**



# kishindo




safi na salama imeimarika vijijini na mijini.

Alisema hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeimarika kutoka wastani wa asilimia 70.1 hadi 77 na mijini asilimia 84 hadi 88 imeimarika kutoka 2020 mpaka Desemba 2022.

Miradi 213 ya usambazaji maji mijini imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi na kunufaisha zaidi ya watu milioni 6.2.

Anasema utekelezaji wa miradi ya maji kwa miji 28 yenye thamani ya Sh. Trilioni 1.48 kuanzia Juni 2022 unaendelea vizuri.

Anasema visima 1,092 vimechimbwa maeneo mbalimbali kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na visima 994 vilivyochimbwa mwaka 2021.

SEKTA YA MAJI
- Huduma za majisafi na usafi na mazingira
- Miradi ya maji zaidi 1,000
- Asilimia 78.5. vijiji vina maji safi na salama

**HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Zuhura anasema kuanzia Machi mwaka 2021 hadi Desemba 2023 usajili wa laini za zimu umeongezeka kutoka zaidi ya milioni 52.3 hadi milioni 70.3.

Anasema watumiaji wa hudua ya Internet wameongezeka kutoka milioni 29 hadi zaidi ya milioni 35.8.

Anasema laini zilizosajiliwa kwa watoa huduma ya fedha imeongezeka kutoka milioni 32.7 hadi zaidi ya milioni 52.8.

Anasema oparesheni ya anuani za makazi imekusanya zaidi ya milioni 12.3 na kusimika nguzo zenye majina ya barabara 229,417, imewezesha vijana 61,783 kupata ajira za muda mfupi na wajasiriamali 9,224 wamenufaika.

Anasema Serikali imeanza ujenzi wa minara 758 katika kata 713, minara 119 kati ya 304 imeongeza nguvu kutoka 2G, 3G na 4G.

**UCHUMI:**

Akizungumzia uchumi, Zuhuru anasema ukuaji wa uchumi mwaka 2023 ulikua kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa 4.7 kwa 2022 ambao umeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za Afrika zenye ukuaji wa kasi ya uchumi.

Aidha anasema mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka kila mwaka Julai 2023 hadi Januari 2024.

Kwa mfano anasema, mapato ya ndani yakijumlishwa na ya Serikali za Mitaa yalifikia Sh. Trilioni 17.19 sawa na asilimia 95.9 ya lengo.

Anasema makusanyo ya kodi ya ndani Desemba 2023 yalivunja rekodi na kufikia Sh. Trilioni 3.05.

**SEKTA YA KILIMO**
- Ongezeko la bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 294 hadi Sh. bilioni 970.
- Ongezeko la uzalishaji wa mazao makuu kutoka tani 898,967 hadi tani milioni 1.29
- Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 18.6 hadi tani milioni 20.4
- Fursa kwa vijana 686 wamepatiwsa mashamba ya uwekezaji katika kilimo
- Ongezeko la uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 50,746 hadi tani 58,807
- Zaidi ya ekari 200,000 zimepatikana Dodoma, Mbeya Kigoma na Kagera
- Mauzo ya mazao ya kilimo kutoka Doal milioni 1.2 hadi Dola milioni 2.3 za Marekani

**SEKTA YA MADINI**
- Ongezeko la soko la madini 42 katika kipindi cha mwaka 2023 hadi Februari, mwaka huu.
- Vituo 100 vya ununuzi wa madini vimeanzishwa
- Sh. bilioni 160.1 zimepatikana kutokana na mrahaba wa mauzo ya madini
- Uwezeshwaji wa mitambo ya kuwahudumia Wachimbaji wadogo
- Ongezeko la ajira kutoka 16,462 mwaka 2022 mpaka 18,475 mwaka jana.

**SEKTA YA AFYA**

KATIKA kipindi cha miaka mitatu tangu kuingia madarakani, Rais Dk. Samia ameendeleza jitihada za kuleta mageuzi na maendeleo katika sekta muhimu ya afya nchini.

Kupitia sera zenye dira thabiti na mikakati inayotekelezeka, Rais Dk. Samia ameimarisha utoaji wa huduma za afya, kukuza ufikiaji wa huduma za afya kwa wananchi wote na kuhakikisha mfumo wa afya unakua endelevu na wenye ufanisi.

Mathalani, Rais Dk. Samia ameimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi (Radiolojia) kwa serikali anayoingoza kununua vifaa tiba vya uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya Sh. bilioni 290.9 ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRHs) na Halmashauri.

**MIFUGO NA UVUVI**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema jumla ya minada ya kisasa 51 imejengwa nchi nzima yenye thamani ya Sh. bilioni 17.5.

Alisema hayo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo wakati ikikagua mradi wa ujenzi wa mnada wa kisasa wa Horohoro uliopo wilayani Mkinga, Mkoa Tanga mwishoni mwa wiki iliyopita.

**TAMISEMI**

"Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani, Tamisemi imepokea zaidi ya Sh. trilioni 6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayogusa wananchi," Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Mohamed Mchengerwa amesema.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

HII NI KERO

## Tudhibiti makelele mitaani

Baadhi ya mitaa ikiwemo Temeke Maganga bado kuna matukio yanayosababisha kelele na kuondoa utulivu majumbani.

Katika mtaa huu wa Maganga maeneo ya Kwa Bi Hafasa, kila wikiendi kuna nyumba kunapigwa mnanda ambao huondoa utulivu mtaani. Mnanda pia hukaribisha vijana wahuni na wezi. Wahusika wawalazimishe wahusika kupeleka starehe zao kwenye kumbi maalumu badala ya wazi ambayo huvutia watoto.





MAONI YA MHARIRI

## Miaka mitatu nchi katika mikono salama

LEO tunaadhimisha miaka mitatu ya uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na jemedari shupavu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alipofariki dunia Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, viatu vyake vilionekana kama vipana sana na barabara mbele yetu ilionekana kama ina vikwazo vingi. Mvaaji wa viatu vyake alitakiwa avivae ghafla na safari iendelee kwenye barabara ngumu kupita.

Lakini, Waswahili wanasema mwenye macho haambiwi tazama wala mwenye masikio haambiwi sikia. Makubwa Rais Dk. Samia ameyafanya, yanajieleza yenyewe au kwa lugha nyepesi, 'kazi yake inaongea'.

Kuanzia kwenye huduma za jamii kama maji, elimu, umeme, miundombinu ya barababara hadi kwenye sekta kama za kilimo, ufugaji, utalii, madini na biashara mambo ni bambam.

Mbali na kuanzisha miradi mipya lukuki, miradi yote mikubwa ambayo ilianzishwa katika Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekelezwa kwa kasi kubwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao sasa umeshaanza kuzalisha megawati 235, mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam ambao tayari umeshaanza kufanyiwa majaribio, ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi mkoani Mwanza ambao umefikia asilimia 80 na ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda hadi Tanga, Tanzania, kutaja kwa uchache.

Rais Dk. Samia pia amejipambanua kwamba uongozi wake umejengwa katika nguzo nne ambazo zinalenga katika kuliunganisha taifa la Tanzania kwenye nyanja zote zikiwemo za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Katika kulifanya taifa kuwa moja lenye kufurahiwa na kila Mtanzania, Rais Dk. Samia amekuwa akiziweka nguzo hizo nne katika falsafa ya "R" nne, ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), Ustahamilivu (Resilience), Mageuzi (Reforms) na Ujenzi Mpya (Rebuild).

Hakuna ubishi kwamba kupitia maridhiano katika nyanja ya siasa ambapo kwa nyakati tofauti amekutana na viongozi wa vyama vya siasa, Rais ameonesha kwamba taifa letu ni la raia huru walio sawa, ambamo kila mmoja anapata fursa kutumia uwezo wake kuendeleza jamii.

Rais Dk. Samia amekuwa akisisitiza umuhimu wa kushirikiana ili kuijenga Tanzania yetu yenye kuaminiana, kuvumiliana na kuheshimiana kwa misingi ya haki na usawa, mambo ambayo yanachangilia kulinda tunu kuu za nchi yetu hususani amani.

Ni vyema Watanzania wakiwemo walioko kwenye vyama vya siasa kufahamu nia hiyo njema ya Rais na kumuunga mkono ikiwa ni pamoja na kuendesha siasa za kistaarabu katika kipindi hiki ambacho mikutano ya kisiasa imeruhusiwa. Wajenge hoja zenye kuwaleta pamoja Watanzania na si kuwagawa, au kufanya watu waichukie serikali yao.

Tunakupongeza Rais Dk. Samia kwa kutimiza miaka mitatu ya kuongeza nchi yetu kwa mafanikio makubwa. Tunakuombea heri na salama katika uongozi wako. Kwa wana CCM, hakuna sababu ya kuwa na fomu zaidi ya moja ya urais mwaka 2025. Fomu ya kugombea urais ni moja tu.


### Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255753333330
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com


JICHO LANGU

Na Dk. Reubeni Lumbagala

## Diplomasia imeimarika sana

IMETIMIA miaka mitatu leo tangu Rais Samia aapishwe kuwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania ili kuwatumikia Watanzania na hatimaye kuendeleza juhudi za kuwaletea maendeleo.

Katika kufanikisha mipango na mikakati ya serikali ya kukuza na kuchochea maendeleo ya nchi na watu wake, Tanzania haina budi kujifunza na kushirikiana na nchi nyingine ndani na nje ya bara la Afrika kwani Tanzania si kisiwa, na ndiyo maana suala la diplomasia, hususani diplomasia ya uchumi limepewa msukumo na msisitizo wa kipekee na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Dk. Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia ameimarisha sana diplomasia na nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Mathalani, baada ya kupishwa kuwa Rais, safari yake ya kwanza ilikuwa nchini Kenya kwa majirani zetu wa karibu.

Huko Rais alipata fursa ya kuhutubia Bunge la nchi hiyo na kupitia mazungumzo na viongozi wa Kenya, vikwazo 64 vya biashara vilivyokuwepo kati ya Tanzania na Kenya vilitatuliwa.

"Wote ni mashahidi malori yalikuwa yanakaa mwezi mzima mpakani Kenya na Tanzania, vifaranga hadi vikachomwa moto na mahindi yalikaa hadi yakaota sumu kuvu. Lakini nilipokwenda tulizungumza tukaondoa vikwazo vyote 64. Sasa hivi biashara ya Kenya na Tanzania imekua kwa kiwango kikubwa. Tena faida imekuja upande wetu," anasema Rais Samia.

Si Kenya pekee, bali pia Rais Samia alisafiri kuelekea nchini Uganda kwa ajili ya utiaji saini mikataba ya utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani,Tanga (EACOP).

Juzi Jumapili ilielezwa kuwa mradi huo wa EACOP umeanza kuleta faida kupitia kodi mbalimbali zinazofikia takribani shilingi bilioni 30 na kuzalisha ajira kwa Watanzania.

Katika kuifungua zaidi Tanzania kimataifa ili kuimarisha diplomasia ya kiuchumi na mataifa mengine, Rais Samia amesafiri katika nchi za Burundi, Ethiopia, Namibia, Malawi, Zimbabwe, Afrika Kusini na Rwanda.

Katika ziara hizi, Rais Samia ameendelea kushawishi wawekezaji na wafanyabiashara kuja kuwekeza Tanzania kutokana na uwepo wa mazingira mazuri na rafiki kwa ajili ya uwekezaji na biashara.

Rais Samia amefanya juhudi kubwa za kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na Marekani, ambapo katika ziara yake nchini humo alikokwenda kwa dhumuni la uzinduzi wa Filamu ya Royal Tour, alishuhudia utiaji saini wa mikataba yenye thamani ya shilingi trilioni 11.

Aidha, Rais Samia pia ameimarisha diplomasia ya kiuchumi na nchi za Ulaya na Umoja wa Falme za Kiarabu. Mathalani, Rais Samia alipozuru Falme za Kiarabu katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara (Dubai Expo 2020), alishiriki utiaji saini wa mikataba ya makubaliano 37 yenye thamani ya Sh trilioni 17. Pia Tanzania imenufaika na msaada wa Sh trilioni 1.17 kutoka Umoja wa Ulaya (EU) ikiwa ni sehemu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kukabiliana na janga la Uviko-19.

Rais Samia pia alipata mwaliko wa kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki duniani na nchi ya Vatican, Papa Francis ili kukuza ushirikiano kati ya Tanzania na Vatican, ushirkiano ulioanza tangu mwaka 1960.

Baada ya Rais Samia kumaliza ziara ya siku mbili Vatican, Februari 13, 2024 aliwasili jijini Oslo nchini Norway kwa ziara ya kitaifa.

Katika ziara hiyo, Rais Samia kupitia wajumbe walioshiriki Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Norway lililofanyika jijini Oslo, aliwaalika na kuwakaribisha wawekezaji kutoka Norway kuja kuwekeza nchini kwenye sekta za gesi, mafuta, nishati mbadala, kilimo na mifuko ya uwekezaji na usafirishaji.

Itoshe kusema, ziara hizi za kidiplomasia alizofanya Rais Samia katika nchi mbalimbali, zina manufaa chanya katika ujenzi wa uchumi na maendeleo ya nchi yetu.

Taarifa iliyotolewa na Kituo cha Uwekezaji (TIC) mwanzoni mwa mwaka ilionesha kwamba mwaka jana, 2023 kituo hicho kilisajili miradi 504 yenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 5.6, sawa na takribani shilingi trilioni 10.

Idadi hiyo ni ongezeko la asilimia zaidi ya 100 ikilinganishwa na miradi 132 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Hakika, miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, diplomasia ya uchumi imeimarika sana na hivyo kusaidia katika kufanikisha mipango mbalimbali ya nchi na hivyo kuharakisha maendeleo ya Watanzania.

# Samia anavyoinyanyua sekta binafsi kuchangia Pato la Taifa

**Na John Ngunge**

KABLA ya miaka mitatu ya sasa, Watanzania wengi walishuhudia jinsi sekta binafsi ilivyokuwa ukipunguza wafanyakazi kutokana na kusuasua kiuendeshaji na mazingira ya uzalishaji kuwa ya jua la utosini.

Joto kali la jua lilisababisha baadhi ya wamiliki wa kampuni binafsi, iwe wa viwandani, mahoteli, migodini, biashara au asasi za kiraia, walilazimika kuchukua hatua ya kuwafuta kazi watumishi wao kutokana na kile walichodai kuwepo kwa mazingira magumu ya uendeshaji.

Sekta binafsi ambayo ilikuwa ikishamiri kwa miaka kadhaa nyuma, taratibu ilikumbana na joto la hali ya hewa lililoifanya kusuasua.

Mathalan, ilikuwa kawaida kuona baadhi ya taasisi za kodi zikifunga kwa kufuli mageti ya kampuni za uzalishaji kwa kile kilichokuwa kikielezwa kuwa wamekwepa kulipa kodi.

Kabla ya kuchukua hatua ya kuwapunguza kazi wafanyakazi wao, baadhi ya wamiliki wa kampuni walidai kuwa sababu ya kufanya hivyo ilitokana na kuwepo kwa makadirio ya kodi kubwa na hivyo kushindwa kufanya biashara kwa faida.

Idadi ya kampuni zilizoendelea kufungwa ilidaiwa kuongezeka na hiyo ilimaanisha vijana wengi kupoteza ajira kiasi cha wengine kujikuta wakitumbukia katika matumizi ya dawa za kulevya na mambo mengine ya hovyo hovyo.

Licha ya historia ya sekta binafsi nchini kuanza mbali, Serikali imekuwa ikitekeleza sera za mageuzi ya uchumi kuanzia miaka ya 1980 kwa lengo la kuimarisha na kuiwezesha kuwa mhimili wa ukuaji wa uchumi.

Maendeleo ya sekta binafsi nchini yalitolewa kwenye wodi mahututi na Hayati Rais Ali Hassan Mwinyi ambaye aliruhusu sekta binafsi kushamiri baada ya miaka mingi uchumi kuendeshwa na sekta ya umma, Safari ya Maisha Yangu, Mwinyi aliyefariki dunia hivi karibuni aliandika:

"Matokeo ya juhudi zote hizi ilikuwa kwamba uchumi ulifungulika na wawekezaji kutoka sekta binafsi wakaanza kuwekeza kwa wingi. Furaha ni kuwa katika miaka kumi niliyopata bahati na heshima kubwa yangu ya kuongoza nchi yetu tuliweka mazingira mazuri na wezeshi zaidi kwa sekta binafsi kutoa mchango wake wa ubunifu, ujasiriamali na mitaji katika kujenga uchumi wa Tanzania na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijami. Na zaidi, misingi tuliyoweka iliwezesha na kurahisishia serikali zilizofuata kufanya makubwa zaidi katika kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi, ya ndani na ya nje, katika kujenga na kuendeleza nchi yetu."

Sera ya Taifa ya Uwekezaji imebainisha malengo mahsusi sita na malengo nane ya kisekta.

Baadhi ya malengo hayo ni kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje; kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi; kuhimiza na kuvutia matumizi ya teknolojia za kisasa katika uwekezaji; kuweka mfumo mzuri na wa wazi wa kisheria; na kuondoa urasimu katika taratibu za upatikanaji wa vibali vya uwekezaji.

Hata hivyo, kiuhalisia mchango wa sekta hiyo katika pato la taifa ulikuwa mdogo, moja ya sababu ikiwa ni utashi kwa waliokuwa wakiisimamia. Ilikuwa ikisuasua na kuchechemea.

Akionesha uelekeo wake kuhusu sekta binafsi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alinukuliwa Aprili 2021 wakati akiwaapisha makatibu wakuu na manaibu makatibu wakuu akisema mazingira ya kufanya biashara nchini ni magumu.

Anasema kwa mujibu wa taarifa za Benki ya Dunia (WB) mazingira ya kufanya biashara ya mwaka 2020 (Doing Business Report 2020), inaonyesha Tanzania ni nchi ya 141, kati ya 190 kwa wepesi wa kufanya biashara. Rwanda ni ya 38 na Kenya ni ya 56.

Lakini mageuzi makubwa yanayoendelea kutekelezwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, yamefanya Watanzania kushuhudia na kuendelea kuona mazingira ya uzalishaji kwa sekta binafsi ikibadilika kwa kasi.

Utashi wa Rais Dk. Samia katika kuweka mazingira safi ya kukua na kushamiri kwa sekta hiyo, kunarejesha heshima iliyopotea.

Thamani ya sekta binafsi kuwa injini ya Uchumi wa Taifa duniani kwa ujumla na Tanzania kwa namna ya pekee, imepewa msukumo mkubwa kivitendo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita ya uongozi wa Rais Dk. Samia.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dk. Doto Biteko, anathibitisha dhamira ya ndani ya Rais Dk. Samia kuhusu sekta binafsi pale anaposema maendeleo ya nchi hayawezi kuletwa na Serikali pekee.

Anasema maendeleo yanaletwa kwa ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi ambayo ni chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi.

Jukumu la serikali katika suala hilo, Dk. Biteko anasema ni kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Anamwelezea Rais Dk. Samia kuwa amejipambanua kama mlezi wa sekta binafsi na hataki kuona wafanyabiashara wanapata misukosuko wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Anasema Rais Samia anayo maono nayo ni kujenga sekta binafsi itakayokuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye pato la Taifa.

Lakini ili kufikia azma hiyo, ni lazima viongozi wengine wahakikishe nia njema ya Rais kwa wafanyabiashara inatekelezwa kwa vitendo na kuacha kuwakwamisha kwa makusudi katika juhudi zao za uwekezaji.

Anaeleza upendo wa Rais Dk. Samia kuwa anataka kuona Watanzania wakiwa kwenye daraja la kwanza katika nchi yao na waweze kufanya uwekezaji ndani na nje ya nchi bila vikwazo vyovyote.

Anawaagiza watendaji wa Serikali kuhakikisha wanailea sekta binafsi na kila mtu atimize wajibu wake kwenye eneo lake.

Anasema kama wewe ni mfanyakazi wa Tanesco na kuna mtu anataka umeme, hakuna haja ya kusubiri kesho kama unaweza kumfungia umeme leo kwani kodi atakayolipa ya umeme na mapato kwa Serikali itakunufaisha na wewe pia.

Moja ya mazingira mazuri ambayo serikali imeweka ni kuboresha mishahara ya wafanyakazi wakiwemo wa sekta binafsi kwa kuweka kima cha chini.

Suala hilo limewekwa kisheria kwa wafanyakazi na waajiri wote wa sekta binafsi kupitia Sheria ya Taasisi za Kazi (Sura ya 300), kuhusu Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara ya Mwaka 2022 iliyoanza kutumika Januari 1, mwaka 2023.

Amri hiyo imekuja baada ya kufutwa amri ya mwaka 2013.

Bila shaka Serikali itaendelea kusimamia na kufanya maboresho ya mishahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi kila mwaka kama inavyofanya kwa watumishi wa umma.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dk. Doto Biteko

> **"Matokeo ya juhudi zote hizi ilikuwa kwamba uchumi ulifungulika na wawekezaji kutoka sekta binafsi wakaanza kuwekeza kwa wingi. Furaha ni kuwa katika miaka kumi niliyopata bahati na heshima kubwa yangu ya kuongoza nchi yetu tuliweka mazingira mazuri na wezeshi zaidi kwa sekta binafsi kutoa mchango wake wa ubunifu, ujasiriamali na mitaji katika kujenga uchumi wa Tanzania na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijami. Na zaidi, misingi tuliyoweka iliwezesha na kurahisishia serikali zilizofuata kufanya makubwa zaidi katika kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi, ya ndani na ya nje, katika kujenga na kuendeleza nchi yetu"**



# Upanuzi wa programu za mafunzo na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi unavyowezesha wananchi kupata ujuzi, kuajirika

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhesh. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele katika kuwezesha wananchi kuwa na ujuzi.

Maono ya Dk. Samia na Serikali yake ni kuwa ujuzi ndio utakaotatua changamoto ya ajira, kuwezesha upatikanaji wa nguvukazi kwa ajili ya wawekezaji, kuongeza tija katika uzalishaji na kusukuma maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla. Kwa maono hayo, jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika ili kuhakikisha wananchi wanapata ujuzi kupitia mafunzo ya ufundi stadi kwenye vyuo vya VETA vilivyopo kote nchini.

Katika kipindi cha miaka mitatu (2021 -2024), Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imeendelea kutoa kipaumbele kwenye elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa kuwaongezea wananchi fursa za kupata ujuzi na stadi za kujiajiri au kuajiriwa. Jitihada zilizofanyika ni pamoja na:-

**Ujenzi na upanuzi wa vyuo vya ufundi stadi**

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, Serikali imewezesha kukamilisha ujenzi wa vyuo 33 vya ufundi stadi nchini, 29 kati yake ni vya ngazi ya wilaya na vinne ngazi ya mkoa. Jumla ya Sh. bilioni 94.5 zimetumika katika kukamilisha ujenzi wa vyuo hivyo.

Ili kutimiza azma yake ya kuhakikisha wilaya zote na mikoa yote inakuwa na vyuo vya VETA, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ya Awamu ya Sita ilitenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 64 na kimoja cha Mkoa wa Songwe. Ujenzi wa vyuo hivyo unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2025 na kuchangia ongezeko la udahili wa wanafunzi 89,700 kwenye vyuo vya VETA.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA. Anthony Kasore, anasema lengo la Serikali ni kuwa na angalau chuo cha VETA kimoja kila wilaya ifikapo mwaka 2025 ili kutoa fursa kwa wananchi kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 inayozungumzia juu ya kuweka mazingira wezeshi kwa kujenga na kukarabati vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza idadi ya wahitimu.

Anasema: "Kwa sasa VETA ina vyuo 80 vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi. Serikali inajenga vyuo vingine 65, lengo ni ifikapo mwaka 2025 kila wilaya iwe na chuo cha ufundi stadi."

**Uongezaji udahili na uhuishaji mitaala**

Katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya vijana 213,803, wamedahiliwa na kupatiwa mafunzo ya ufundi stadi kwenye vyuo vya VETA, ambapo idadi ya wadahiliwa kwenye kozi za muda mrefu imeongezeka kutoka wanafunzi 13,491 mwaka 2021 hadi 22,155 mwaka 2024.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa pamoja na viongozi wengine wa Kitaifa wakati akiweka Jiwe la Msingi Chuo cha VETA Wilaya ya Igunga mkoani Tabora Oktoba 17, mwaka jana.



Mkurugenzi wa VETA, CPA. Anthony Kasore

Ili kuhakikisha mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa yanawiana na mahitaji halisi ya soko la ajira, VETA imekuwa ikihuisha mitaala mara kwa mara. Maboresho hayo yanaenda sambamba na uandaaji wa mitaala mipya pale kunapokuwa na uanzishwaji wa programu mpya za mafunzo kufuatia taarifa za mahitaji ya soko la ajira.

Katika kipindi cha mwaka 2021 na 2024, jumla ya mitaala 55 ilihuishwa au kuandaliwa katika sekta za umeme, magari, mitambo, kilimo, ukarimu, usafirishaji, biashara, nguo, madini na urembo.

**Uboreshaji sekta isiyo rasmi kupitia programu maalum**

Ilani ya CCM ya mwaka 2020 imeainisha uwezeshaji vijana, wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri kwa kuwapatia mafunzo na stadi za ujasiriamali na usimamizi wa shughuli za kiuchumi miongoni mwa mikakati ya kupambana na umaskini.

VETA imeendelea kutekeleza programu mahsusi zinazolenga kuwezesha wananchi kujipatia stadi za ujasiriamali na kuwawezesha kurasimisha shughuli zao ili kujiongezea kipato.

*** Programu ya Mafunzo ya Kukuza Ujasiriamali katika Sekta isiyo rasmi (Integrated Training for Entrepreneurship Promotion - INTEP).**

Kupitia programu hii, mafunzo hutolewa kwa wajasiriamali kwa lengo la kuboresha ujuzi wao na maarifa ili waongeze tija na kunufaika zaidi na shughuli zao za kiuchumi. Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, jumla ya wajasiriamali 4,931 kati yao 3,299 ni wanawake wamenufaika na mafunzo hayo hapa nchini.

*** Mpango wa Utambuzi na Urasimishaji Ujuzi uliopatikana nje ya Mfumo Rasmi wa Mafunzo (Recognition of Prior Learning - RPL).**

Kupitia mpango huu, mhusika (mwanagenzi) hufanyiwa tathmini ya ujuzi wake ili kutambua umahiri alionao, mapungufu yake na hatimaye VETA kumpatia mafunzo kisha kumtunuku cheti.

Miongoni mwa mafanikio katika utekelezaji wa RPL, VETA ilifanya tathmini ya ujuzi wa mafundi wanaoshiriki kwenye ujenzi katika mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

Hatua hiyo inalenga kutambulisha ujuzi wa wanagenzi hao katika soko la ajira kupitia vyeti na kuwasaidia kupata kazi nyingine mara baada ya miradi kukamilika. Jumla ya wanagenzi 1,275 wamefanyiwa tathmini na kutunukiwa vyeti katika mradi wa SGR (238) na JNHPP (1037).

**Uwezeshaji wa makundi mbalimbali ya vijana**

Msemo maarufu wa vijana ni nguvu Kazi ya Taifa unaakisi umuhimu wa vijana katika kutenda kazi na namna ambavyo vijana wanategemewa kufanya kazi ili kujenga Taifa.

Ili vijana hawa waweze kuwa nguvukazi ya Taifa ni lazima wawe na ujuzi na maarifa ya kutenda kazi. Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 nchini Tanzania yalibainisha kuwa, asilimia 34.5 ya Watanzania ni vijana.

Serikali imeendelea kubuni programu mbalimbali kwa kushirikiana na wadau zenye kuwajengea ujuzi vijana ambazo zinafadhiliwa na Serikali na wabia wa maendeleo.

*** Mradi wa kukuza Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo Tanzania (Employment and Skills for Development Tanzania - E4DT)**

Kupitia mradi huu jumla ya vijana 4,295 katika Mikoa ya Lindi, Manyara, Dodoma na Dar es Salaam walinufaika na mafunzo ya ufundi stadi kwenye fani za ufundi bomba wa majumbani, ufundi bomba viwandani, ufundi wa uchomeleaji vyuma viwandani na majumbani pamoja na ufundi wa Mekatroniki. Mradi huu ulitekelezwa na VETA kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Misaada na Maendeleo la Korea (KOICA).

Wanufaika wa mradi huu walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na kushiriki shindano la mtaji mbegu, ambapo jumla ya miradi 67 yenye vijana 171 ilishinda mtaji mbegu ya vitendea kazi vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200.

*** Programu ya uanagenzi chini ya ufadhili wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,**

Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Programu hii inalenga kuwapatia ujuzi vijana kupitia mafunzo ya ufundi stadi yanayohusisha kijana kutumia asilimia 40 ya muda wake kwa masomo ya nadharia darasani na asilimia 60 ya muda wake kwa masomo ya vitendo sehemu ya kazi. Mafunzo hayo yanatolewa kwa muda wa miezi sita na yanafadhiliwa na Serikali kwa asilimia 100. Tangu kuanzishwa kwa programu hii mwaka 2019, jumla ya vijana 11,591 wamenufaika na mafunzo hayo kupitia vyuo vya VETA.

**Hali ya ajira kwa wahitimu wa VETA**

Kwa mujibu wa Taarifa ya Ufuatiliaji wa Wahitimu wa Ufundi Stadi (Trace Study) uliofanywa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) mwaka 2023, ukihusisha wahitimu wa miaka mitano kutoka 2017 hadi 2021, imebainika kuwa asilimia 67.7 ya wahitimu wa ufundi stadi wameajirika.

CPA Kasore anaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa kipaumbele kwenye elimu na mafunzo ya ufundi stadi na kuahidi kuwa VETA itaendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa ufanisi na kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanapata ujuzi na kushiriki vyema kwenye shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

# VETA Dodoma inavyokuza ujasiriamali, uwezo wa kuajirika

MIONGONI mwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwezesha vijana, wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri kwa kuwapatia mafunzo na stadi za ujasiriamali na usimamizi wa shughuli za kiuchumi na kuwezeshwa kurasimisha shughuli zao.

Sambamba na hilo, Serikali pia inataka kuona kuwa miradi mikubwa ya kimkakati inaajiri vijana wengi zaidi wa Kitanzania.

Hayo yote yanaweza kufanikiwa kwa ufanisi mkubwa kupitia utoaji wa elimu na mafunzo ya kukuza ujuzi na stadi mbalimbali kwa vijana Watanzania.

Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dodoma ( VETA Dodoma) kimebeba ajenda ya utekelezaji wa mpango huo kupitia programu mbalimbali kwa kushirikiana na wadau.

### UJENGAJI UMAHIRI KUPITIA MRADI WA E4D

Mradi wa E4D ni miongoni mwa programu iliyowajengea vijana uwezo na umahiri mkubwa wa ujuzi na ujasiriamali ni mradi wa Ujuzi na Ajira kwa Maendeleo, yaani Employment and Skills for Development (E4D).

Tanzania ni miongoni mwa nchi sita za Barani Afrika zilizotekeleza mradi wa E4D. Lengo la E4D ni kukuza ajira kwa vijana katika miradi ya uwekezaji inayohitaji nguvu kazi kubwa na pia kuwawezesha kujiajiri.

Mradi huu ulifadhiliwa na Wizara ya Shirikisho la Ujerumani ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleola Norway (Norad), Umoja wa Ulaya (EU), na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Korea (KOICA).

Mkuu cha Chuo cha VETA Dodoma, Stanslaus Ntibara anasema kupitia mradi huu, vyuo vya VETA viliendesha mafunzo ya miezi minne minne ya ufundi stadi katika Fani za Uchomeleaji Vyuma Viwandani (Industrial Welding), Ufundi Bomba wa Viwandani na Majumbani (Industrial and Domestic plumbing) na Mekatroniki (Mechatronics) kwa vijana takribani 4,000 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Mafunzo haya yalitolewa katika vyuo vinne (4) vya VETA, ambavyo ni Dodoma, wanafunzi 2,200, Lindi wanafunzi 800, Manyara wanafunzi 700 na Kipawa wanafunzi 300.

"Kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi, chuo cha Dodoma kiliruhusiwa kuwa na vyuo vinne saidizi (VETA Iringa, Singida, Mikumi na Dodoma)," anafafanua.

Aidha, katika mradi huu walengwa walipata fursa ya kushiriki mafunzo maalumu ya ujasiriamali yanayoambatana na shindano la kuwapata washindi kwa ajili ya kuatamiwa na hatimaye kujiajiri.

Mashindano ya miradi ya ujasiriamali yalihusisha vijana 235 (wa kiume 151 na wa kike 84), katika jumla ya miradi 101. Jumla ya miradi iliyoshinda ni 67 ikiwahusisha vijana 171 (wa kiume 116 na wa kike 55).

"Tunajivunia kuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huu. Ushirikiano na wadau wa maendeleo katika mradi huu umeturuhusu kupata rasilimali muhimu, teknolojia, na ujuziwa kisasa unaosaidia kufanikisha malengo ya muda mrefu katika utoaji wa mafunzo," Ntibara anasema.

Anasema VETA ilivuka lengo la utekelezaji wa huo kwa kufundisha wanafunzi 4295 ukilinganisha na wanafunzi 4000 waliokuwa wamelengwa. Aidha, Chuo cha VETA Dodoma pamoja na vyuo vyake visaidizi vilitoa mafunzo kwa wanafunzi 2,217.

Ntibara anasema, licha ya kutoa vijana mahiri na wenye stadi za ujasiriamali, utekelezaji wa mradi huo umekuwa na manufaa mengine mengi kwa VETA.

Anayataja manufaa hayo kuwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya mafunzo, ambapo mashine na vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Shilingi takribani bilioni 2.28 vilinunuliwa; uandaaji mitaala na ujengeaji uwezo wakufunzi ambapo jumla ya walimu 36 walipata mafunzo.

### MRADI WA TANIPAC

Huu ni mradi wa mafunzo ya kuongeza usalama wa chakula na kupunguza upotevu wa mazao. Chuo cha VETA Dodoma ni miongoni mwa vyuo vilivyotekeleza mradi huu wa Kudhibiti Sumu kuvu nchini Tanzania, kwa Kiingereza: "Tanzania Initiatives for Preventing Aflatoxin Contamination - TANIPAC)".

Mradi huo ulitekelezwa na VETA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa miaka mitano, 2019 hadi 2023 na ulilenga kushughulikia changamoto ya usalama wa chakula, hususani sumu kuvu, katika mnyororo wa thamani wa mazao ya karanga na mahindi. Vilevile, mradi huo ulilenga kupunguza upotevu wa mavuno.

VETA ilifundisha utengenezaji wa vihenge vya chuma (metal silos) kwa wananchi katika mikoa 10 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mkuu wa Chuo, Ntibara, anasema, chini ya mradi huo, Chuo cha VETA Dodoma kiliweza kutoa mafunzo kwa vijana 60 wa wilaya za Bahi, Chemba, Kongwa na Kondoa.

Ntibara anahitimisha kwa kuwahakikishia wananchi kuwa chuo cha VETA Dodoma kitaendelea kuimarisha huduma zake na kuendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wa maendeleo ili kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata ujuzi unaowawezesha kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.



Baadhi ya wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi katika chuo cha VETA Dodoma kupitia mradi wa kukuza ajira na ujuzi kwa maendeleo ya Afrika (E4D) wakiwa na vifaa walivyowezeshwa kama mtaji mbegu ili kuwawezesha kujiajiri.

# Mafunzo ya ufundi stadi chuo cha VETA Manyara yanavyochagiza Kilimo Biashara

SERIKALI ya Awamu ya Sita iliweka bayana dhamira yake ya kuhakikisha vijana wanashiriki kwenye kilimo na wanaendesha sekta hiyo kwa njia ya kisasa ili kilimo hicho kiwe na tija. Jitihada mbalimbali zimefanyika ikiwemo uanzishwaji wa programu maalum za kukuza kilimo sambamba na kutenga maeneo maalumu ya kilimo kwa ajili ya vijana.

Katika kuinua tija kwenye sekta hiyo, Serikali pia imeendelea kutekeleza programu mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wake wa ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa program hizo ni utoaji wa mafunzo kwa vijana, ili vijana hao wawe na ujuzi utakaowawezesha kuendesha kilimo kibiashara na kukuza uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

Miradi iliyotekelezwa kupitia VETA na manufaa yake ni pamoja na: Mradi wa kuthibiti Sumukuvu Tanzania uliosaidia kuongeza usalama wa chakula na kupunguza upotevu wa mavuno.

VETA ilishirikiana na Wizara ya Kilimo katika mradi huo kutoa mafunzo ya ujuzi wa teknolojia ya utengenezaji wa vihenge vya chuma (Metal Silos) kwa ajili ya kuhifadhia nafaka katika ngazi ya kaya. Lengo ni kutatua changamoto ya usalama wa chakula, hususani udhibiti wa sumukuvu na hivyo kuwaongezea vijana uwezo wa kiuchumi na kuongeza kipato cha wakulima kwa kupunguza upotevu wa mavuno. Jumla ya vijana 420 katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Manyara, Kigoma, Tabora, Ruvuma, Mtwara, Morogoro na Geita wamenufika na mafunzo hayo.

Utekelezaji wa programu hii umechangia pia katika utekelezaji wa Ilani ya CCM kuhusu Kuwezesha Uwekezaji katika Kilimo Biashara, kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya 37, kipengele C na Kipengele kidogo (b).

Aidha, katika kuhakikisha uendelevu wa kutumia ujuzi huo kwa ajira na kusaidia kudhibiti sumukuvu na upotevu wa mavuno, vijana wote 420 walionufaika na mafunzo ya utengenezaji wa vihenge vya chuma, walipatiwa bure vifaa vya uchomeleaji na uungaji vyuma (Welding and Metal Fabrication Tool Kit), vikijumuisha: mashine za kuchomelea (Welding Mashine), mashine za kukatia vyuma (Angle Grinder), mashine za kutobolea (Drilling Machine), Divider, vifaa vya kupimia (Tape Measure), punch, misumeno (Hacksaw), kifaa cha kupimia kona, nyuzi 90 (Try-square), na miwani kinga (Safety Goggle).

Mkuu wa Chuo cha VETA Manyara, Nansanga Godwin anasema chuo hicho kilitoa mafunzo ya utengenezaji vihenge kwa wananchi 60 katika Wilaya za Babati, Kiteto na Kondoa na kutoa pongezi kwa Serikali kwa kuwezesha utoaji wa mafunzo ya utengenezaji wa vihenge ambavyo vitasaidia kuhakikisha usalama wa chakula nchini.

Mmoja wa wahitimu wa mafunzo hayo katika Chuo cha VETA Manyara, Yassin Surumbu, anasema utaalamu alioupata wa kutengeneza vihenge na vifaa alivyopatiwa baada ya kuhitimu vimemwezesha kutoa suluhisho kwa jamii yake kwenye uhifadhi wa mazao ambapo awali mazao hayo yalikuwa yakiharibika na kukosa soko.

Anasema, mafunzo hayo pia yamempatia fursa ya kujiajiri na kujipatia kipato na kwamba ujuzi alioupata umemwezesha kutoa ujuzi kwa kuwashirikisha vijana wenzake kwenye kazi hiyo.

Mpango wa Uanagenzi Pacha uliowezesha vijana kuajirika katika makampuni ya kilimo

Serikali kupitia VETA inatambua umuhimu wa kuzalisha nguvukazi mahiri na yenye ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira na imeendelea kuwashirikisha waajiri katika utoaji mafunzo. Mfumo wa Uanagenzi Pacha unahusisha utoaji mafunzo mahali pa kazi ambako mhusika (mwanagenzi) hupata ujuzi kwa vitendo na katika mazingira halisia na chuoni ambako mwanagenzi hujifunza nadharia na vitendo kwenye karakana za chuo.

Mpango huu unawahakikishia waajiri upatikanaji wa wafanyakazi wenye ujuzi unaohitajika kwa kupunguza tofauti kati ya matarajio ya mahitaji ya soko la ajira au na mafunzo yanayotolewa vyuoni, hatimaye kuongeza tija katika uzalishaji.

VETA inaendesha mpango huu kwa kushirikiana na viwanda na makampuni mbalimbali ambapo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2013, zaidi ya wanagenzi 1,200 wamenufaika na mpango huo huku makampuni 252 yakishiriki katika utekelezaji wa mafunzo katika fani za Ufundi Magari, Ufundi Umeme, Hoteli, Ukarimu na Utalii, Ufundi wa Zana za Kilimo na Ufundi Bomba.


Chuo cha VETA Manyara ni miongoni mwa vyuo vinavyotekeleza mpango huu kupitia fani ya Ufundi wa Zana za Kilimo, ambapo tangu kuanza kwake mwaka 2019, jumla ya wanagenzi 133 walidahiliwa chuoni hapo.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Nansanga Godwin anasema wahitimu wa mpango huo katika chuo hicho wamefikia 67 na kwa sasa wapo kwenye maeneo mbalimbali wakitumia ujuzi wao katika kubuni na kutengeneza zana mbalimbali za kilimo kwa ajili ya kuleta ufanisi kwenye sekta hiyo.

**KOZI ZINAZOTOLEWA KATIKA CHUO CHA VETA MANYARA**

- Ufundi wa Magari (Motor Vehicle Mechanics)
- Uashi (Masonry and Bricklaying)
- Useremala (Carpentry and Joinery)
- Ufundi wa Mitambo na Zana za Kilimo (Agromechanics)
- Ufundi wa Elektroniki (Electronics)
- Uhazili (Secretarial and Computer Application)
- Ufundi Umeme (Electrical installation)
- Uungaji na Uundaji vyuma (Welding and Metal Fabrication)
- Wasaidizi wa Maabara (Laborarort Assistant)

*MAWASILIANO*
*Simu:*
*027 2975113 / 0717582148*
*Barua pepe:*
*manyararvtsc@veta.go.tz*



Nansanga Godwin, Mkuu wa Chuo cha VETA Manyara

**Wahitimu wa mpango huo katika chuo hicho wamefikia 67 na kwa sasa wapo kwenye maeneo mbalimbali wakitumia ujuzi wao katika kubuni na kutengeneza zana mbalimbali za kilimo kwa ajili ya kuleta ufanisi kwenye sekta hiyo.**



# VETA Moshi inavyowezesha vijana kuajirika katika miradi mikubwa

SERIKALI imeweka mpango wa kutoa mafunzo ya kukuza ujuzi na stadi mbalimbali za kazi kwa nguvukazi ya Taifa katika sekta za kipaumbele na kuhakikisha kuwa miradi mikubwa ya kimkakati inaajiri vijana wengi zaidi wa Kitanzania.

Katika kuchangia kwenye mpango huo, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imekuwa ikishirikiana na wadau kutoa mafunzo yanayolenga kuwapa Watanzania ujuzi mahsusi kwa ajili ya sekta maalumu na miradi mikubwa.

**UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA MOSHI**

Chuo cha VETA Moshi ni miongoni mwa vyuo vya VETA nchini vinavyotoa mafunzo mahsusi kwa sekta na miradi maalumu.

**MAFUNZO KWA AJILI YA SEKTA YA MADINI**

Mafunzo ya uanagenzi kwa ajili ya Sekta ya Madini yajulikanayo kama Integrated Mining Technical Training (IMTT) yalianzishwa kwa nia ya kuandaa nguvukazi mahiri ya vijana wa Kitanzania ili kufanya kazi kwenye migodi mbalimbali ya madini nchini.

Mafunzo haya yalianza mwaka 2009 kufuatia mahitaji ya mafundi mahiri katika sekta ya madini ambapo mradi ulianzishwa kwa ushirikiano kati ya VETA na kampuni za uchimbaji wa madini.

Miongoni mwa kampuni hizo ni Barrick kupitia kampuni yake tanzu ya Bulyanhulu Gold Mine Limited na Anglo-gold Ashanti kupitia kampuni yake tanzu ya Geita Gold Mine Limited. Haya yanafanyika chini ya uratibu wa Chemba ya Madini Tanzania (TCM). Washirika wameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na chuo kinakaribisha washiriki na wadau zaidi katika kushirikiana na chuo.

Katika mradi huo, mafunzo yamekuwa yakigusa maeneo yenye uhitaji mkubwa katika uchimbaji madini ikiwemo ufundi wa mitambo mikubwa (heavy moving equipment mechanics); ufundi umeme; ufundi umeme wa magari; uungaji wa vyuma vizito (plater welding); na ufundi mitambo (fitting and machining).

Mfumo wa mafunzo ni wa uanagenzi ambao unahusisha mafunzo chuoni na mafunzo mahala pa kazi (kwenye kampuni mbalimbali) kwa njia ya kupokezana (Block release program).

Katika mfumo huu, nusu ya mafunzo ya mwanagenzi hutolewa mahala pa kazi na nusu ya mafunzo hutolewa chuoni.

Mfumo huu huwezesha wanagenzi kuwa na uzoefu na uwezo mkubwa wa kazi kwa kuwa muda mwingi hujifunza kwa mazoezi ya vitendo katika mazingira halisi ya kazi.

Kwa hiyo washiriki wa programu wanaomaliza huwa na umahiri mkubwa wa kukubalika kwa waajiri maeneo mbalimbali.

Mkuu wa Chuo cha VETA Moshi, Ramadhani Mataka anasema, hadi kufikia Desemba 2023, mradi wa IMTT ulikuwa umefanikiwa kutoa mafunzo kwa wanagenzi 1,500, na kwamba kati ya hao takribani asilimia 95 wameweza kujiajiri au kuajiriwa katika kampuni za uchimbaji madini, taasisi za umma na kampuni mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa sasa wanagenzi 332 wanaendelea na mafunzo.

"Licha kunufaisha vijana wengi, mradi huo umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha karakana, kuimarisha utoaji mafunzo ya usalama mahala pa kazi, kuimarisha uhusiano wa chuo na wadau ikiwemo TCM, migodi ya madini na sekta zingine," anasema.

Mataka anasema kutokana na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mradi huo, mwaka huu (2024) yamesainiwa tena makubaliano (MoU) ya kuhuisha mradi huo kwa miaka mitatu mingine.



Mwanafunzi wa fani ya Uchomeleaji na Uungaji Vyuma, akiwa katika mazoezi ya vitendo kwenye karakana ya chuo cha VETA Moshi.

**BOMBA LA MAFUTA**

Mafunzo ya ujuzi pia yanatolewa na chuo kwa ajili ya vijana wa Kitanzania kushiriki kwenye mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) kwa nia ya kuhakikisha vijana wa Kitanzania wananufaika na fursa za ajira kwenye ujenzi wa bomba hilo.

VETA ilisaini makubaliano (MoU) na kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP Limited), Septemba 14, 2023, kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vijana wa Kitanzania kupitia chuo cha VETA Moshi.

Bomba hili linajengwa kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kutoka Hoima, nchini Uganda ambako yanazalishwa, hadi katika bandari inayojengwa kwa ajili ya kupokelea mafuta, Chongoleani, Tanga, nchini Tanzania.

Mafuta hayo yanatazamiwa kuuzwa kwenye masoko mbalimbali ulimwenguni. Ni bomba la urefu wa kilometa 1,443 ambapo asilimia 80 ya urefu wake iko Tanzania.

Meneja wa Ajira na Mafunzo wa EACOP Limited, Laurent Stephane anasema mafunzo hayo yatakayotolewa kwenye chuo cha VETA Moshi yataendeshwa kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza itakuwa ya miezi sita ambayo itakuwa ya mafunzo ya stadi za msingi.

Awamu ya pili ni ya mafunzo ya umahiri katika fani, pia yanatolewa kwa miezi sita. Mafunzo hayo yanatolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Petroli Kigumba Uganda (Uganda Petroleum Institute Kigumba-UPIK).

Awamu ya tatu inahusisha mafunzo kwa vitendo sehemu za kazi.

Akizungumza kuhusu ushirikiano wakati wa utiaji saini uliofanyika katika Hoteli ya Coral Beach, jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, alisema, "Makubaliano haya yanabainisha fursa kubwa kwa vijana wetu kuweza kupata stadi zenye manufaa, kuwawezesha kuajirika, hususani katika mradi wa bomba la mafuta ghafi na kwenye maeneo mengine ya kiuchumi nchini."

Aliongeza: "Ni fursa pia kwetu (VETA) kuongeza nguvu katika juhudi zetu za kufikia dira yetu ya kuwa na Tanzania yenye mafundi stadi, mahiri na wa kutosha ili kushiriki katika maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii."

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mwendeshaji wa EACOP Limited, Martin Tiffen, alisema kwamba ushirikiano huo ni muhimu katika kuwezesha kufikia matokeo mazuri ya mradi.

"Kwa kufanya kazi pamoja, tutahakikisha kuwa vijana wa Tanzania wameandaliwa vyema ili kunufaika na fursa zinazotokana na bomba la mafuta ghafi," alisema.

Aliongeza kwamba, Ushirikiano kati ya VETA na EACOP pia utaleta faida za kiuchumi na kijamii kwa vijana wa Kitanzania.

Vijana watakapopata mafunzo na kushiriki katika ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, watapata ajira na fursa za kiuchumi ambazo zitawawezesha kuboresha maisha yao na kuchangia katika maendeleo ya jamii zao.


CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA CHA MKOA WA DAR ES SALAAM
VETA
TANGAZO LA KOZI FUPI ZA KUENDESHA MITAMBO YA UJENZI
MOTOR GRADER, EXCAVATOR & WHEEL LOADER
MUDA: MIEZI MIWILI
ADA YA MAFUNZO: TSH 1,120,000
GHARAMA YA FOMU: TSH 5000
UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA
www.veta.go.tz

# Ushirikiano wa Chuo cha VETA Kihonda na wadau wachangia kuboresha sekta za uchukuzi na kilimo



Mkuu wa Chuo cha VETA Kihonda, Theresia Ibrahimu



> Chuo cha VETA Kihonda kimebobea katika kutoa mafunzo ya udereva kuanzia udereva wa awali mpaka magari makubwa.

SEKTA ya uchukuzi ina umuhimu wa kipekee na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi kiuchumi. Hata hivyo, miongoni mwa changamoto katika sekta hiyo ni uhaba wa nguvukazi mahiri, hususani madereva wenye uwezo na weledi katika usafirishaji. Wengi tumeshuhudia ajali nyingi za magari ya mizigo barabarani, ambazo aghalabu husababisha hasara kubwa kutokana na uharibifu wa magari; upotevu wa bidhaa zilizokuwa zikisafirishwa na wakati mwingine madhara na vifo vya watu.

Chuo cha VETA Kihonda kimebobea katika kutoa mafunzo ya udereva kuanzia udereva wa awali mpaka magari makubwa.

Mkuu wa Chuo cha VETA Kihonda, Theresia Ibrahimu, anasema ili kusaidia sekta ya uchukuzi na kuhakikisha kuwa ina madereva mahiri Chuo cha VETA Kihonda kiliamua kutanua wigo wa huduma zake za mafunzo ambapo badala ya kuishia kutoa mafunzo chuoni kwake pekee kilianzisha mafunzo ya nje ya chuo (Outreach). Mafunzo hayo yamekuwa yakifanyika kwa kushirikiana na makampuni na taasisi mbalimbali.

Anasema kupitia mpango huo chuo kimeweza kushirikiana na makampuni na taasisi takribani 22 kutoka sekta binafsi na za umma katika kutoa mafunzo kwa madereva wa magari makubwa. Baadhi ya makampuni yaliyoshiriki katika mpango huo ni pamoja na

GSM, World Oil, A.K Transport, Merzario, Blue Coast, Lake Trans, TKT, CIMC, Goldwish Transport, Delina, XYZ Transport na Camel Transport.

Anasema mpango wa mafunzo nje ya chuo na ndani ya chuo umeweza kuleta manufaa makubwa katika sekta ya uchukuzi ikiwemo kupunguza ajali za barabarani, kuokoa mali na maisha ya watu, kufungua nafasi za ajira katika sekta ya uchukuzi na kuongeza tija katika makampuni mbalimbali ya usafirishaji na utoaji wa huduma zinazohitaji usafirishaji wa mizigo na bidhaa.

Vilevile, mafunzo yamewezesha kuimarisha ujuzi katika urekibishaji wa hitilafu ndogo ndogo kwenye magari kwa njia salama, hivyo kupunguza uharibifu wa mali unaoweza kutokea kutokana na hitilafu ndogo ndogo au makosa ya udereva ambayo pia unaweza kupelekea ajali. Pia madereva waliofunzwa vizuri wameweza kupata ajira kwa urahisi kwa sababu ya mahitaji ya mara kwa mara ya madereva wa magari makubwa.

"Madereva waliopata mafunzo kupitia mpango huo wameweza kuwa na ujuzi mzuri wa kuendesha magari makubwa kwa usalama na kujihami, hivyo kupunguza idadi ya ajali zinazosababishwa na makosa ya udereva. Pia tumewajengea uzalendo kwa kuhakikisha magari yao yanakuwa na bima kila wakati. Jambo hili linathibitika kutoka kwenye taarifa mbalimbali zinazotufikia kutoka askari wa usalama barabarani," Theresia Moshi amefafanua.

Anaeleza kuwa kwa ujumla wake, mafunzo ya udereva wa ngazi mbalimbali kupitia chuoni na nje ya chuo yametolewa kwa wananchi 4,848 katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kwamba taarifa zimeonesha kuwa idadi ya wanawake katika sekta ya usafirishaji imeongezeka tofauti na hapo awali.

Theresia anasema kuwa mafunzo ya udereva yanayotolewa na Chuo cha VETA Kihonda yanajumuisha elimu juu ya utunzaji wa barabara, taa na alama za miongozo, hivyo upimaji wa uzito pamoja na udereva unaozingatia sheria zinazoongoza usafirishaji imezingatiwa katika mafunzo.

Mafunzo ya katika kilimo kwa kushirikiana na wadau Chuo cha VETA Kihonda ni miongoni mwa vyuo vya VETA vinavyoendesha mafunzo ya ufundi wa zana za kilimo kwa mfumo wa uanagenzi. Mpango wa mafunzo hayo unafanyika kwa ushirikiano kati ya VETA na Serikali ya Ujerumani inatoa mafunzo kwa kushirikiana na makapuni wadau katika sekta ya kilimo. Katika mafunzo haya wanafunzi wanasoma kwa mfumo wa kupokezana (Block Release), ambapo kunakuwa na kipindi mafunzo chuoni kwa wiki kadhaa na kipindi mafunzo sehemu ya kazi. Mafunzo ya aina hii yamewavutia wengi kwani mwanafunzi (ambaye hapa anaitwa mwanagenzi) akiwa sehemu ya kazi anajifunza kwa vitendo katika mazingira halisi ya kazi.

"Kinachofurahisha zaidi ni mwanafunzi kuzalisha zao ambalo anashuhudia likienda sokoni na kuongeza kipato cha kampuni," anasema Theresia.

Kupitia mpango huu, Chuo cha VETA Kihonda kimekuwa kikiendesha mafunzo hayo kwa kushirikiana na kampuni na taasisi zikiwemo Kilombelo Sugar Co. Ltd, Mkulazi Sugar Co. Ltd, Bagamoyo Sugar Co. Ltd, ASAS, Mtibwa Sugar Co. Ltd, AgriCom, SUMA JKT, SUA, Mbalali Highland Estate.

Theresia Ibrahimu anaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kipaumbele katika mafunzo ya ufundi stadi ambayo imewatia hamasa wawekezaji na wadau mbalimbali wa elimu kushikiana na chuo cha VETA Kihonda ili kuzalisha mafundi mahiri wanaokubalika ndani na nje ya Tanzania.

Anawaalika wadau kuendelea kuungana na chuo cha VETA Kihonda kuunga mkono jitihada Rais Dk. Samia ili kuzalisha mafundi stadi kwa ajiri ya maendeleo ya Taifa la Tanzania.

# Watalii waongezeka maradufu, mapato yapanda, Tanzania yatangazika zaidi

Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) yenye dhima ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, kuhamasisha uendelezaji wa miundombinu ya utalii, kufanya tafiti za utalii na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa Sekta ya Utalii, imeshuhudia mafanikio lukuki katika miaka hii mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Katika makala haya tunaorodhesha baadhi ya mafanikio hayo.

**ONGEZEKO LA WATALII**

Kumekuwa na ongezeko la idadi ya watalii wa kimataifa nchini kutoka 620,867 mwaka 2020 hadi watalii 1,808,205 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 191.

Hatua hii imewezesha Tanzania kutambuliwa na Shirika la Utalii Duniani kama nchi ya pili Afrika na ya 12 duniani kwa ukuaji wa utalii.

**MAPATO YAPAA**

Mapato yatokanayo na shughuli za utalii pia yameongezeka hadi kufikia Dola za Marekani Bilioni 3.3 mwaka 2023 kutoka Dola za Marekani Bilioni 0.7 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 371.

**THE ROYAL TOUR**

Programu mahususi ya Tanzania The Royal Tour iliyoasisiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ili kutangaza vivutio vyetu vya utalii na fursa za uwekezaji imeongeza chachu ya watalii kutembelea Tanzania na kuvutia uwekezaji.

Kadhalika, Bodi ya Utalii imeratibu kurekodiwa kwa filamu ijulikanayo kama Kijiji cha Milele ambayo imemhusisha pia Rais Samia na muigizaji maarufu kutoka China, Jin Dong inayotazamiwa kuchochea ujio wa watalii zaidi kutoka China na Bara la Asia kwa ujumla.

**UTANGAZAJI UTALII KIDIJITI**

Utangazaji wa utalii kidijiti umeimarika ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa kituo cha Destination Digital Marketing Command Centre (DDMCC) kwa lengo hilo.

Hatua hiyo imewezesha kuongezeka kwa wafuatiliaji wa taarifa za vivutio vya utalii zinazotolewa na Bodi ya Utalii nchini na hadi kufikia Februari 2024, kwa mfano, idadi ya wafuatiliaji katika mitandao ya kijamii ilifikia 301,718.

**MAZAO YA UTALII**

Bodi ya Utalii pia imeimarisha utangazaji na uendelezaji wa mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo Utalii wa Meli, Utalii wa Fukwe, na Utalii wa Mikutano na Matukio.

Ni katika muktadha huo, meli mbalimbali za kitalii ikwemo Seabourn Sojourn, La Jacques Cartier Ponant & Coral Geographer zilizuru Tanzania kutoka Nchi za Marekani, Australia, Norway na Uholanzi zikiwa na watalii zaidi ya 3,145.

**UTALII WA TRENI**

Bodi ya Utalii imefanikiwa kuimarisha zao jipya la utalii wa treni ambapo kwa kushirikiana na wadau imeratibu ujio wa treni za kifahari za Kampuni ya Rovos kutoka Nchini Afrika Kusini. Aidha, watalii wanaokuja na treni hiyo hutembelea vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo Makumbusho ya Taifa, maeneo ya kihistoria, hifadhi za Taifa, na maeneo ya fukwe.

**UTALII WA MIKUTANO**

Utalii wa Mikutano na Matukio ambao umeainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020 2025) kama zao la utalii la kimkakati katika kufikia watalii milioni tano unaendelea kuimarishwa.

Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa matukio mbalimbali ya kimataifa ikiwemo Onesho la kwanza la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Oktoba 2021 Jijini Arusha.

Vilevile, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani uliofanyikaOktoba, 2022 Jijini Arusha.

Matukio haya na mengine kadhaa ambayo hayajaorodheshwa hapa yalichangia kwa kiasi kikubwa kutangaza nchi yetu kimataifa sambamba na kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi.

**MAZAO YA UTALII KIJIOGRAFIA**

Bodi ya Utalii imefanikiwa kupanua wigo wa mazao ya utalii kijiografia kwa kutangaza na kuendeleza utalii katika mikoa ya kusini, hatua iliyoimarisha utangazaji wa vivutio vilivyopo katika mikoa hiyo ikiwemo hifadhi za taifa za Mikumi, Nyerere na Ruaha, Mapori ya Akiba Selous na Mpanga Kipengele, Fukwe za Bahari ya Hindi na ziwa Nyasa, Eneo la Ziwa Ngosi, na maeneo mbalimbali ya kihistoria ikiwemo Mji wa Kilwa ambao ni sehemu ya Urithi wa Dunia.

**NCHI KUPATA TUZO MBALIMBALI**

Tanzania imeendelea kutambuliwa kimataifa na kupata tuzo mbalimbali. Kwa uchache sana tuzo hizo ni ya Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa Hifadhi Bora Barani Afrika kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2023; Tanzania kuwa Nchi ya saba miongoni mwa nchi 18 zilizo bora kutembelewa kiutalii kwa mwaka 2022 na Hifadhi ya Taifa Serengeti kuorodheshwa kama eneo maridhawa kutembelewa kwa mwaka 2023.

Halikadhalika, Bodi ya Utalii Tanzania ilikuwa mshindi wa kwanza wa taasisi zinazotangaza utalii Barani Afrika (Africa s Leading Tourism Board) huku Hifadhi ya Ngorongoro ikiwa mshindi wa kivutio bora Barani Afrika.

**KUTANGAZA UTALII KWENYE MAONESHO**

Bodi ya Utalii imeshiriki na kutangaza utalii katika nchi ambazo ni masoko yetu ya utalii kupitia Maonesho, Matukio na Misafara ya Kutangaza Utalii (Roadshows) ikiwemo Dubai Expo (UAE), ITB Berlin (Ujerumani), WTM London (Uingereza), East African Regional Tourism Expo EARTE (Kenya & Burundi), IFTM Top Resa (Ufaransa), My Tanzania Roadshow katika nchi za Ulaya Magharibi na Mashariki, kutaja kwa uchache.

Kadhalika, Bodi ya Utalii imeshiriki katika makongamano ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo katika Sekta ya Utalii.

Miongoni mwa makongamano ambayo Bodi ya Utalii ilishiriki ni pamoja na Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Indonesia, Italia, na Austria. Pia Bodi imeshiriki katika mikutano ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa 66 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Afrika (66th UNWTO CAF Meeting) uliofanyika Mauritius, Mkutano Mkuu wa 25 wa Shirika la Utalii Duniani (25th UNWTO General Assembly) uliofanyika Uzbekistan, na Mkutano wa Baraza la Safari na Utalii (WTTC) uliofanyika Rwanda.

**ONESHO LA S!TE**

Bodi ya Utalii imefanikiwa kurejesha upya Onesho la Utalii la Kimataifa la S!TE (Swahili International Tourism Expo) lililofanyika mwaka 2022 na 2023 katika Ukumbi wa Mlimani City Jijini Dar es Salaam. Onesho hilo halikufanyika mwaka 2020 na 2021 kutokana na uwepo wa Janga la UVIKO-19.

**UTALII WA NDANI**

Bodi ya Utalii imetangaza utalii wa ndani kupitia maonesho, matukio na kampeni mbalimbali zilizolenga kuwahamasisha Watanzania kutembelea vivutio vyetu vya utalii.

Maonesho, matukio na kampeni hizo ni pamoja na Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Mwl. Julius Nyerere (Sababa), Maonesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane), Serengeti Marathon, NBC Marathon, Kilimanjaro Marathon, Mpalano Festival, National Cultural Festival, Karibu Kusini, Kizimkazi Festival, Mafia Festival, Z-Summit (Zanzibar) na mengine lukuki mfano wa hayo.

**ZIARA ZA KIMKAKATI**

Bodi ya Utalii imefanikiwa kuanzisha ziara za kimkakati zenye lengo la kukutana na wawekezaji wakubwa kwenye Sekta ya Utalii kwenye nchi ambazo ni masoko makubwa ya utalii duniani.

**TANZANIA KUSAJILIWA KIMATAIFA**

Bodi ya Utalii imefanikiwa kuisajili Tanzania katika mashirika na vyama mbalimbali vya utalii duniani kwa lengo la kushirikiana katika kutangaza utalii wetu na kuvutia watalii zaidi kutembelea Tanzania. Miongoni mwa vyama na mashirika hayo ni pamoja na Baraza la Safari na Utalii Duniani (WTTC) na Chama cha Wakala wa Utalii Nchini Marekani.

**UTALII KUPITIA MICHEZO**

Utangazaji utalii kupitia michezo ya kimataifa pia umeimarika. Mathalani, Bodi ya Utalii ilifanikiwa kutangaza utalii wa Tanzania wakati wa Mashindano ya Kombe la Dunia (World Cup) yaliyofanyika Nchini Qatar mwaka 2022.

Kadhalika, Bodi ya Utalii imefanikiwa kutangaza vivutio vya utalii na kauli mbiu ya 'Tanzania Unforgettable!' wakati wa mchezo wa mashindano ya Klabu Bingwa Afrika (CAF Championship League) na Mapinduzi Cup, kutaja kwa uchache.

Hii ni bila kusahau Mchezo wa Tennis uliofanyika katika Hifadhi ya Taifa Serengeti na kuhudhuriwa na wacheza tennis mahiri duniani na watalii 83 kutoka Marekani.

**USHIRIKIANO NA MASHIRIKA YA NDEGE**

Bodi pia imeimarisha ushirikiano na mashirika mbalimbali ya ndege kwa lengo la kutangaza utalii wetu kupitia mashirika hayo.

**KUJENGEA MAWAKALA UZOEFU**

Bodi ya Utalii imewajengea uzoefu mawakala wa biashara za utalii, waandishi wa habari, na watu mashuhuri kutoka nchi ambazo ni masoko yetu ya utalii kupitia ziara za mafunzo ili waweze kuitangaza Tanzania ipasavyo.



# Mageuzi makubwa MSD

## ●Upatikanaji wa bidhaa wapaa kwa asilimia 31
## ●Mapato yaongezeka kutoka bil. 320/- hadi 373/-
## ●Matumizi nayo yapungua kwa Sh. bilioni 16

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeifanyia mageuzi makubwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kwenye mifumo ya ununuzi, usambazaji wa bidhaa za afya, kuhifadhi na kuzalisha.

Mtendaji Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, aliyeteuliwa kushika nafasi hiyo Aprili 14, 2022, amesema mageuzi makubwa yaliyofanywa na Rais Dk. Samia, yanadhihirisha namna Serikali anayoiongoza ilivyodhamiria kumaliza tatizo la uhaba wa bidhaa za afya nchini.

Kwa mujibu wa Tukai, yako mambo kadhaa ambayo MSD inajivunia kwa sasa katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia.

Tukai anafafanua kuwa mambo hayo ni pamoja na ongezeko kubwa la upatikanaji wa bidhaa kutoka asilimia 51 mpaka asilimia 82 kwa miaka miwili.

"Huu ni ufanisi mkubwa ndani ya muda mfupi," anasema Tukai na kufafanua kuwa mwaka 2021/2022, mapato ya MSD yalikuwa Sh. bilioni 320, lakini kwa mwaka 2022/2023, yameongezeka na kufikia Sh. bilioni 373.

Aidha, anasema mwaka wa fedha, 2023/24 kufikia Februari, tayari wamekusanya Sh. bilioni 225 na kwamba upatikanaji wa vifaa tiba umeongezeka pia.

Vilevile, anasema katika uchambuzi linganishi wa ufanisi wa nusu mwaka kwa nusu mwaka, inaonesha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, MSD ilikusanya Sh. bilioni 159. Hii inamaanisha kwamba wamekusanya Sh. bilioni 106 zaidi ya kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

### MATUMIZI

Matumizi ya MSD kwa sasa ni Sh. bilioni 66 tu ikiwa ni tofauti na kipindi cha nyuma ambapo matumizi yalikuwa ni Sh. bilioni 82.

### KUTAMBULIKA NJE YA WATUMIAJI WA DAWA, VIFAA TIBA

Katika vigezo vilivyowekwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (IGA), MSD wamekuwa washindi wa 10 kutokana na kuthibika kukidhi vigezo vilivyowekwa na mamlaka hiyo.

Aidha, kwa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), MSD wamekuwa washindi wa kwanza katika kundi la walipaji kodi wa kati kwani nao hulipa kodi, hununua na kutoa huduma.

Kabla ya mageuzi makubwa haya kufanyika, MSD ilikuwa ikikabiliwa na upungufu wa dawa nchini takriban asilimia 50, na hivyo hospitali kukosa bidhaa za afya.

Maboresho makubwa MSD yaliyofanywa na Rais Dk. Samia, yameifanya taasisi hiyo kwa sasa kutoa huduma za kuridhisha kwa wananchi.

Baada ya Rais Dk. Samia kumteua Tukai kuwa Mtendaji Mkuu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwaondoa Wakurugenzi na hivyo MSD yenye majukumu ya uzalishaji, uhifadhi, ununuzi na usambazaji ikawa na sura mpya ya watendaji.

Tukai alipoingia ofisini, aliweka mikakati ya kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata dawa.

Tukai anasema menejimenti ilianza kwa kukagua hospitali na vituo vya afya vyote ili kujua kiasi cha dawa kilichopo na kiini cha upungufu.

Kadhalika, Tukai anasema walilenga kufahamu mahitaji halisi ya kila kituo cha kutolea huduma za afya na hivyo wakawajibika kufanya kazi usiku na mchana.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu huyo, walibaini muundo wa MSD wa kuwa na wakurugenzi na mameneja makao makuu bila kuzifikia ngazi za kanda na mikoa, ulikuwa na upungufu.

"Niliagiza kanda zichukue majukumu ya kuendesha MSD. Meneja wengi wa kanda walibadilishwa, tulipeleka wapya na kuwawaita watu wa kanda na kuwaongezea majukumu ya kusimamia kanda na kuwasisitiza kuwa wasiwe na hofu kuhusu bajeti, watupe mahitaji yao ya kanda," anasema Tukai.

Anasema mfumo huu ni wazi kwamba unaleta ushidani baina ya mameneja wa kanda na hivyo kuongeza mapato, jambo lililowezesha malengo kuvuka na kufikia asilimia 100 na zaidi.

Kadhalika, anasema mfumo huo umedhihirisha mahitaji halisi ambayo yameifanya MSD kusambaza dawa mikoani kila baada ya miezi miwili yaani mara sita kwa mwaka mzima.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan



Mtendaji Mkuu wa MSD, Mavere Tukai

Anafafanua kuwa utaratibu wa awali, zamani, MSD ilikuwa inasambaza dawa kila baada ya miezi mitatu yaani mara nne kwa mwaka, hali iliyosababisha dawa kutopatikana kwa baadhi ya maeneo hivyo mfumo huo mpya, umewapa mwanga kwani MSD kwa wakati huu imesogezwa karibu na wananchi.

"Kanda zinafahamu mahitaji yao halisi na kwamba tumefikia asilimia 84 ya usambazaji wa dawa. Tunajivunia kwa hilo na Wizara ya Afya, umetuwezesha kufanya kazi nzuri," anasema Tukai.

Anasema kati ya mwaka 2021/2022, MSD ilipoteza biashara ya Sh. bilioni 500 kwa kutowahudumia wateja kwa mujibu wa kampuni ya Deloitte Consulting iliyopewa kandarasi ya kufanya uchambuzi.

"Deloitte Consulting, ilingundua maeneo takriban sita kwamba MSD haifanyi vizuri na hivyo kushauri uwezo wa kifedha, uwe endelevu kwani haukuwa imara kutokana na sababu mbalimbali," anasisitiza Tukai.

Aidha, alisema baadhi ya masuala mengine yaliyopendekezwa na kufanyiwa kazi katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia ni kuwa na mtaji wa biashara, udhibiti mzuri wa fedha zinazopatikana zitumike kwa ufanisi.

Tukai anasema MSD imejipanga kuongeza vyanzo vya mapato, kupunguza madeni, gharama za uendeshaji na kukakikisha kwamba inakuza mapato.

Anasema kwa sasa, MSD kwa sasa ununuzi unafanyika kwa kutumia teknolojia.

"Tunazishirikisha Balozi zetu za nje ya nchi kwa kutafuta wazalishaji. Tunapata bidhaa bora kwa bei nafuu. Baadhi ya dawa na vifaa tiba tunapata kutoka India, China, Misri, Korea na Algeria,"anasema Tukai.

Aidha, anasema mikataba ya wazabuni kwa sasa ni imara kuliko miaka ya nyuma kwani wameweka utaratibu wa kuwapa washitiri mikataba ya uhakika wa muda mrefu.

### MAFUNZO KWA WATUMISHI

Tukai anasema baadhi ya watumishi wa MSD wanaosoma kozi za muda mfupi na muda mrefu kwa gharama ya mwajiri lengo likiwa ni kuhakikisha taasisi ina watu sahihi.

Hata hivyo, Tukai anasema MSD zipo changamoto kadhaa katika ghala za kuhifadhia dawa kwani kwa sasa uwezo wake ni asilimia 36 huku sekta binafsi ina maghala yenye uwezo wa kuhifadhi asilimia 20 ya dawa na vifaa tiba vinavyotumika nchini hivyo kufanya uwezo wa kuhifadhi bidhaa hizo kuwa asilimia 56 nchini. Changamoto hii inaifanya nchi isiweze kununua mzigo mkubwa wa dawa na vifaa tiba kwa wakati mmoja.

Tukai anafafanua kuwa maghala ya Mtwara, Iringa na Kilimanjaro, hayana uwezo wa kuhifadhi dawa za miezi miwili. Dar es Salaam na Kagera MSD wanakodisha maghala ya kuhifadhi dawa na vifaa tiba. Kagera wanakodisha Hospitali ya Muleba.

"Mwanza inahudumia watu milioni 11. Ghala halina uwezo wa kuhudumia miezi miwili. Ujenzi wa maghala mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2012 na idadi ya watu imeongezeka kwa asilimia 37, vituo vya afya vimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 70," anasdema Tukai.

Tukai anasema katika kukabiliana na hali hiyo, MSD imeanza kujenga maghala katika baadhi ya Kanda ambapo awamu ya kKwanza inajenga Mtwara na Dodoma ambayo itakuwa kiungo cha mikoa jirani ili kupunguza umbali.

Anaongeza kuwa MSD pia imeunda vitengo vipya kikiwamo cha mikataba na kuruhusu sekta binafsi kutoka Makao Makuu kwenda kwenye kanda.

Aidha, Tukai anasema MSD imekusudia kulinda mazingira ambapo katika maghala, wanatumia mabati yanayopitisha mwanga kuepusha matumizi ya taa mchana, kutumia umeme wa jua, betri za kutunza umeme, taa rafiki wa mazingira, magari kupunguza urefu wa safari, kutumia magari ya umeme na ya kutumia gesi na kwamba yatapunguza matumizi ya umeme kwa asilimia 70.

Anasema Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), umeipa MSD ushindi wa pili kitaifa.

Tukai anasema serikali imekubali kuipa MSD mtaji wa Sh. bililioni 561.5, na wanamshukuru Rais Dk. Samia kwa kuiunga mkono katika kazi ya kuipa uhai taasisi sambamba na Waziri wa Afya, Ummy.

" Viongozi wote akiwamo Katibu Mkuu na wote tunaofanya nao kazi, wameonesha dhamira ya dhati kuhakikisha Watanzania wanapata dawa za uhakika na kwa wakati," anasema.

Hata hivyo, Mtendaji Mkuu huyo wa MSD, amewataka wanaopewa dawa zikiwamo hospitali kubwa, wqalipe kwa wakati ili taasisi hiyo iendelee kufanya kazi zake kwa ufanisi.

# Huduma za tiba ki
# bobezi zaimarika

## ■ Zavutia utalii tiba nchini ■ Ni kutokana na uwekezaji ka

**Na Hamisi Kibari**

WAKATI tunapata uhuru mwaka 1961, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alilitangazia Taifa maadui watatu wakubwa ambao alisema hatuna budi kupambana nao. Maadui hao ni ujinga, maradhi na umasikini.

Kimsingi, tangu wakati wa Mwalimu Nyerere, nchi imeendelea kupambana na maadui hao na hakuna ubishi kwamba nchi yetu imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya maadui hao.

Katika makala haya tunaangalia mapambano dhidi ya adui maradhi na hususani namna Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan inavyopambana na adui huyu. Wananchi wanapokuwa wanaumwa, hawawezi kuzalisha mali na familia hutumia muda na gharama kubwa kuuguza.

Pengine katika awamu zote, ni katika awamu ya Rais Samia ambayo serikali imejenga, kumalizia au kuboresha majengo ya kisasa katika hospitali zetu, kusomesha wataalamu na kununua vifaa tiba vya kisasa ambavyo vimewezesha sasa tiba nyingi ambazo watu walikuwa wakizifuata nje ya nchi kuzipata hapahapa nyumbani.

### KUSOGEZA HUDUMA KARIBU NA WANANCHI

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani, Serikali imefanya kazi kubwa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na kuzifanya kuwa bora na nafuu zaidi kwa kujenga vituo vya kutolea huduma za afya, kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba pamoja na kuajiri watumishi wapya.

Uboreshaji huo umewezesha huduma ambazo awali zilikuwa zikipatikana zaidi katika hospitali za mikoa au hospitali za wilaya kama X-ray na upasuaji mkubwa kushushwa na kupatikana kwenye vituo vya afya.

Aidha, uwekezaji huo umepunguza umbali wa mwananchi kuzifikia huduma za afya ambapo sasa wanaweza kuzipata kwa wastani wa chini ya kilomita tano. Uimarishaji wa huduma za wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu na huduma za dharura umepunguza rufani kwenda hospitali za juu.

Serikali ya Awamu ya Sita pia imekuwa ikiwaagiza madaktari kutoka Hospitali ya Taifa, hospitali za kanda na hospitali za rufaa na za mikoa kwenda kutoa huduma za kibingwa na bobezi kwenye hospitali za halmashauri kwa njia ya mkoba (outreach services) ili kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi

Katika mpango huo, waganga wakuu wa halmashauri nchini wanatakiwa kutumia mapato ya ndani ya hospitali zao kuwezesha madaktari bingwa na bobezi kufika katika hospitali za wilaya na kutoa huduma za kibingwa na bobezi kwa wananchi.

### HUDUMA ZA KIBINGWA

Uwekezaji mkubwa ambao umewekezwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Upanga na Mloganzila, umefanya Muhimbili kuwa alama halisi ya matibabu, hususani ya kibingwa nchini na hata nje ya mipaka ya Tanzania.

Matibabu ya kibingwa na vifaa tiba vya kisasa vyenye ubora vinaokoa maisha ya Watanzania na mamilioni ya fedha zilizokuwa zikipelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kutibu Watanzania.

Kupitia juhudi za Rais Samia, mwaka 2022/2023, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilipokea fedha za Uviko-19, shilingi bilioni 11 na milioni 800 ambazo zimewekezwa katika maeneo tofauti ikiwemo vifaa vya uchunguzi, wataalamu wabobezi na vifaa tiba katika wodi mbalimbali zikiwemo za wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu.

Hali hii inaifanya Muhimbili kuwa na vifaa tiba vingi vya kisasa kulinganisha na hospitali nyingine katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Kwa sasa, madaktari na wahudumu wa afya wanajivunia kufanya kazi katika mazingira bora huku upatikanaji wa dawa kwa sasa ukiwa ni asilimia 98 na zile za kuandikiwa dawa kisha kuambiwa ukanunue duka fulani kuendelea kubaki historia.

### KUREKEBISHA MAUMBO

Kurekebisha maumbo, maarufu kama 'upasuaji rekebishi' ni moja ya huduma ambayo haikuwepo nchini lakini sasa inafanywa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila.

Tiba hii inahusisha upasuaji wa



> **Gharama za huduma hiyo ni shilingi milioni 3.5 hadi shilingi milioni nne tu wakati nje ya nchi ni zaidi ya shilingi milioni 15.**



Timu ya wataalamu MNH-Mloganzila wakiongozwa na Dkt. Eric Muhumba (wakwanza kulia) wakimuwekea mtu mwenye uzito uliopitiliza puto maalumu litakalomsaidia kupunguza uzito..jpg



# bingwa na maradufu

## tika majengo, vifaa tiba, watala



Mkurugenzi MNH, Profesa Mohamed Janabi

kibingwa katika kupunguza uzito na kurekebisha viungo. Katika kupunguza uzito, watalaamu wanapunguza nafasi ya chakula na kuna aina tatu ya kufikia urekebishaji huu. Mojawapo ni kupunguza tumbo lenyewe, yaani kukata sehemu ya tumbo.

Mkuu wa Idara ya Upasuaji wa Muhimbili-Mloganzila, Dk. Erick Muhumba, anasema aina ya pili ni kuvuka sehemu ya kuhifadhia chakula na kwenda kwenye utumbo mdogo moja kwa moja na kwamba hii ni njia ya kisasa zaidi inayofanywa bila upasuaji wa mwili. Anasema endscopia inaingizwa mdomoni hadi ndani ya tumbo, utumbo mdogo unashonwa na kuwa na sehemu ndogo.

"Tumbo likizidi mafuta tunapunguza kama sehemu ya mwili. Kama mtu anataka kurekebisha matiti kuwa madogo au makubwa inarekebishwa na nyama za mikono."

Anaongeza: "Huduma hii kwa Mloganzila gharama yake itakuwa nafuu zaidi kuliko kwenda nje ya nchi kwa hiyo tumerahisisha, watu wanapata huduma kwa ukaribu na urahisi, hakuna tofauti na kwenda kupata huduma kama hii nje ambako ukienda gharama ni kubwa," anasema.

Anaainisha kuwa gharama za upasuaji zinatofautiana kuanzia Sh milioni 15 hadi Sh milioni 22.5 ambapo inategemea na mtu na aina ya upasuaji.

### KUPUNGUZA UZITO KWA KUTUMIA PUTO

Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila pia ina huduma ambayo ni nadra kuikuta kwingineko katika ukanda huu wa Afrika Mashariki ya kuweka puto maalumu kwenye tumbo la chakula kwa watu wenye uzito uliopitiliza (intragastic ballon) ambayo inasaidia kupunguza nafasi kwenye tumbo la chakula hivyo kusababisha mtu kula kidogo, jambo ambalo linapelekea kupungua uzito.

Gharama za huduma hiyo ni shilingi milioni 3.5 hadi shilingi milioni nne tu wakati nje ya nchi ni zaidi ya shilingi milioni 15.

Daktari Bingwa wa Upasuaji, Dk. Eric Muhumba anasema huduma ya kuweka puto hufanyika kwa dakika 20 ambapo hufanyika kwa kutumia mashine ya endoscopia, hivyo haihusishi upasuaji wa aina yoyote.

Dk. Eric ameongeza kuwa puto likishawekwa tumboni hukaa kwa muda kati ya miezi sita hadi nane ndipo hutolewa na baada ya hapo mtu huyo atakuwa ameshajenga utamaduni wa kula kidogo hivyo atakuwa amepuguza uzito wa kutosha.

### UPASUAJI REKEBISHI WA MACHO

Ukiacha upasuaji unaolenga urembo au kupunguza uzito kama ambavyo tumeshaona, Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila pia imeanza kufanya upasuaji rekebishi wa macho.

Kumbukumbu zinaonesha kwamba wiki iliyopita tu madaktari wa hospitali hiyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa bobezi kutoka Sudan waliwafanyia wagonjwa 12 upasuaji huo.

Wagonjwa hao walikuwa na changamoto mbalimbali za macho. Baadhi ya matatizo yao yalikuwa uvimbe nje ya jicho, makengeza kwa watu wazima, majeraha yaliyotokana na ajali au makovu ya muda mrefu, kutoka machozi kwa muda mrefu kutokana na kuziba kwa njia za machozi na changamoto ya vifuniko vya macho.

Akizungumza baada ya upasuaji huo, Dk. Muhumba anasema: "Lengo la hospitali yetu ni kuendelea kutoa huduma za kibingwa bobezi ili kuwawezesha wananchi wengi kupata huduma za matibabu ubingwa bobezi hapahapa nchini. Hospitali imejipanga vyema kuhakikisha huduma hizi zinakua endelevu."

Ili kupeleka ujuzi zaidi wa upasuaji huo katika hospitali nyingine, madaktari wazawa kutoka hospitali nyingine pia walishiriki kwenye upasuaji huo. Madkatarei hao ni wa kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma; Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Pwani, Tumbi; Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Mtwara, Ligula; Hospitali ya Kanda Mbeya pamoja na Hospitali ya St. Benedict, Lindi.

### MTAMBO WA KUTIBU MAGONJWA ZAIDI YA 10

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pia ina mtambo unaotumia hewa tiba yenye mgandamizo wa oksijeni (Hyperbaric Medicine Treatment) kwa ajili ya kutibu magonjwa zaidi ya 10.

Inaelezwa kwamba Tanzania ni nchi ya kwanza katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na ya pili Kusini mwa Jangwa la Sahara kutumia mtambao huo.

Mkurugenzi MNH, Profesa Mohamed Janabi anasema kupitia matibabu hayo mgonjwa huingizwa kwenye kifaa maalumu na kupatiwa tiba kupitia hewa tiba ya oksijeni iliyogandamizwa kwa asilimia 100.

Kwa mujibu wa Janabi, wagonjwa wanaonufaika na mtambo huo ni wale wenye vidonda sugu ambavyo matibabu mengine yameshindikana kama wagonjwa wa sukari (diabetic foot), walioathirika na moshi baada ya kuungua na moto (carbon monoxide poisoning) na waliopata changamoto za upungufu wa oksijeni mwilini kama waliozama kwenye maji baharini n.k (decompression syndrome).

Prof. Janabi anataja wagonjwa wengine kuwa ni pamoja na walioungua na moto (acute thermal injury), wenye upungufu mkubwa wa damu ambao kwa njia moja au nyingine hawawezi kuongezewa damu (severe anemia), waliopata ajali na kupata majeraha mwilini yasiyopona (Crush injury, compartment syndrome and other acute traumatic ischemia) na wagonjwa wenye maambukizi kwenye mifupa isiyopona (Refractory osteomyelitis)

Anasema wagonjwa wengine wanaoweza kunufaika na mtambo huo ni waliopata mionzi na kusababisha sehemu zilizopata tiba mionzi kuathitika ikiwemo wenye saratani za koo, njia ya chakula na wale wenye tezi dume (delayed radiation injury both soft tissue and bony necrosis), waliofanyiwa upasuaji na kuwekewa/ kupandikiziwa sehemu ya miili yao (compromised grafts and flaps), wenye changamoto ya kusikia ambao vipimo vimeshindwa kuonyesha tatizo (idiopathic sudden sensorineural loss), wenye tatizo la usaha kwenye ubongo (intracranial abscess), wenye changamoto ya oksijeni kwenye mishipa ya damu (arterial insufficiencies) na watoto wenye usonji (autisim).

### KUTIBU MAUMIVU SUGU BILA UPASUAJI

Tumeona huduma chache tu za kibingwa ambazo zamani zilikuwa hazipatikani kabisa nchini lakini zinazotolewa na Hospitali ya Taifa Muhimbili Upanga au Mloganzila.

Lakini Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) nayo imekuwa ikiandika historia katika matibabu ya kibingwa na moja ya huduma hizo ni matibabu ya maumivu sugu ya mgongo na kichwa bila upasuaji.

Huduma hiyo ilianzishwa hivi karibuni hapa nchini kwa ushirikiano wa Taasisi ya MOI na Hospitali ya Yashoda ya India.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface anasema wameanzisha huduma hiyo ili kuendelea kutekeleza agizo la Serikali ya Awamu ya Sita la kuhakikisha Tanzania inakuwa kituo cha utalii wa matibabu (Medical Tourism).

"Kama mnavyofahamu Mheshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan ana msukumo mkubwa wa kuifanya nchi yetu kuwa kitovu cha utalii wa matibabu katika Ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini, hivyo kuanza kwa huduma hii ni sehemu ya mkakati wetu wa kutekeleza kwa vitendo maono hayo ya Mheshimiwa Rais," anasema Dk. Boniface.

Huduma nyingine ya kibingwa miongoni mwa nyingi pale MOI ni kufanya matibabu ya kibingwa ya upasuaji wa magoti na bega kwa njia ya matundu (arthroscopy). Hatua hiyo imeelezwa kwamba imekuwa ikiokoa mabilioni ya pesa kama wagonjwa hao wangelazimika kwenda kutibiwa nje ya nchi.

### TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE

Kama kuna taasisi ambayo imekuwa ikifanya makubwa katika kuja na tiba za kisasa za kibingwa na bobezi ni Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Baadhi ya tiba hizo ni upasuaji mdogo wa moyo wa kubadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa damu (Aortic Valve) bila kufungua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implantation procedure – TAVI)

### HOSPITALI YA BENJAMINI MKAPA

Hospitali ya Benjamini Mkapa pia imekuwa pia ikitoa matibabu ya kibingwa ya kupandikiza figo na magonjwa yanayohusiana na figo na mkojo, magonjwa ya ndani, magonjwa ya moyo, haemotolijia, tiba zinazohusiana na mifupa, kupandikiza uboho na mengine lukuki.

### TANZANIA KUWA KITOVU CHA TIBA UTALII

Serikali inasema kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika sekta ya afya nchini na Serikali ya Awamu ya Sita, unaendelea kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha Tiba Utalii kwa kutoa huduma za afya kwa wagonjwa maalumu wa ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anasema kutokana na uwekezaji katika miundombinu, vifaa tiba na wataalamu, MOI pekee imefanikiwa kupunguza rufaa za wagonjwa kwenda nje ya nchi ambapo hadi sasa asiliamia 99 ya huduma za mifupa pamoja na asilimia 97 ya huduma za kibingwa za ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu zinapatikana hapa nchini.

Taarifa iliyowahi kutolewa karibuni inaonesha kwamba wagonjwa zaidi ya 300, kutoka nje ya nchi walikuwa wamepatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge anataja nchi wanazotoka wagonjwa hao kuwa ni Somalia, Malawi, Kenya, Rwanda, Visiwa vya Comoro, Ethiopia, Burundi, Armenia, Norway na Uingereza.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa Muhimbili Mloganzila, Dk. Julieth Magandi anasema uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali pamoja na maboresho makubwa yaliyofanywa na uongozi wa hospitali ikiwemo uanzishwaji wa huduma za kibingwa, umekuwa unavutia raia wa kigeni kufika Mloganzila kufuata huduma.

"Tumeanzisha huduma za kibingwa, lakini pia tumeboresha huduma kwa wateja. Kuna dawati la huduma kwa wateja ambalo linafanya kazi saa 24 ili kuhakikisha wateja wetu wanahudumiwa vizuri, jambo hili limevutia raia wa nchi mbalimbali ikiwemo Kenya, Afrika Kusini na Malawi kufuata huduma Mloganzila" anasema Dk. Magandi.

Tanzania pia imekuwa ikipeleka madaktari wake bingwa na bobezi kwenda kutibu katika nchi za jirani. Mathalani, Serikali imewahi kutuma madaktari bingwa 12 kwenda nchini Zambia kutoa huduma za kibingwa za matibabu ya moyo kwa watoto, hii ikiwa ni sehemu ya kuendelea kutanua wigo wa tiba utalii na kukuza mahusiano baina ya nchi hizi mbili.



# Ametoa uwanja sawa siasa za ushindani

**Na Dk. Reubeni Lumbagala**

LEO Machi 19, 2024, niungane na watanzania wenzangu kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake tangu alipoapishwa rasmi Machi 19, 2021 kuwa Rais wa Tanzania kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli kilichotokea Machi 17, 2021.

Kufuatia kuapishwa kwake, Rais Samia aliyekuwa Makamu wa Rais wa wakati huo, akashika usukani wa kuwa Rais kamili kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuendeleza gurudumu la maendeleo ya nchi.

Kimsingi, tangu Rais Samia aingie madarakani, amefanya mengi mazuri huku akigusa nyanja zote za maisha yaani kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Makala haya yanaangazia nyanja ya kisiasa ambapo Rais Samia ameitendea haki sana na huku akithibitisha kwa vitendo bila kuacha shaka ya aina yeyote kuwa yeye ni mwanademokrasia wa kweli kuanzia maneno hadi vitendo.

Na hii inatokana na ukweli kuwa Rais Samia anaelewa vyema umuhimu wa demokrasia katika kufanikisha agenda ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Ni katika demokrasia hiyo ambapo chama tawala kinakumbushwa vyema kuhusu uwajibikaji kupitia sauti zinazopazwa na vyama vya upinzani na hatimaye kujirekebisha na kufanya vyema zaidi kwa manufaa ya wananchi.

Chama tawala, yaani Chama Cha Mapinduzi (CCM) kina nafasi ya kufanya vyema zaidi kupitia hoja zinapoibuliwa na vyama na upinzani, na hivyo kunufaika zaidi kwa kufanyia kazi hoja hizo na hatimaye kuendelea kuongoza nchi kwani kufanyia kazi mawazo yanayotolewa na wapinzani, kunasaidia kutatua kero vinazogusa maisha ya wananchi.

Januari 3, 2023, Rais Samia akizungumza na viongozi wakuu wa vyama vya siasa vya upinzani Tanzania, alitangaza kufuta zuio na hatimaye kuruhusu tena mikutano ya hadhara.

Akiwa Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Samia alisema: "Nianze na la mikutano ya hadhara, hii ni haki kwa sheria zetu. Ni haki ya vyama kufanya mikutano yao ya hadhara na kwa bahati taarifa zote mbili zimeibuka kama ni jambo muhimu sana. Uwepo wangu leo mbele yenu ni kuja kufanya ruhusa, kuja kutangaza lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara sasa linaondoka."

Ikumbukwe pia kuwa uhai wa vyama vya siasa ni pamoja na kuendesha shughuli za kisiasa kila siku ambapo mikutano ya kisiasa ni jukwaa muhimu la kujinadani na kuzungumzia masuala muhimu ya kitaifa ili kutafuta majibu ya pamoja kwa ustawi wa maendeleo ya wananchi.

Kutokana na zuio lililokuwepo, lilikwamisha vyama vya siasa kufanya shughuli zake kwa uhuru, na ndiyo maana Rais Samia akaondoa zuio hilo ili kutoa uwanja sawa wa siasa za ushindani kati ya chama tawala na vyama vya upinzani.

Lakini tuwe tunakumbuka kwamba zuio la mikutano lililowekwa na Serikali ya Awamu ya Tano lilikuwa na sababu pia hata kama pengine zilionekana kama zinaminya demokrasia lakini zina mafunzo yake kwetu kama Watanzania.

Huko nyuma ilianza kuonekana kama nchi iko kwenye kampeni za uchaguzi muda wote! Yaani tunamaliza leo uchaguzi na kesho watu wanaanza mikutano isiyokwisha kiasi cha kutoipa utulivu serikali iliyochaguliwa na wananchi. Pia unajiuliza, wanaoandamana na kujaa kwenye mikutano, wanafanya kazi ya kuzalisha saa ngapi?

Pia kulijitokeza mtindo wa wanasiasa kuokota skendo za viongozi walioko madarakani kwenye korido, zisizo na ushahidi wowote na kuzifanya ajenda kwenye mikutano yao na baadhi ya vyombo vya habari kuzibeba zilivyo bila kuzitafutia usahihi. Ndio maana baadhi ya wanasiasa wa upinzani walijikuta mahakamani na wengine kukosa ushahidi wa madai yao huku pia baadhi ya magazeti yakifungiwa.

Lakini magazeti hayo yamefunguliwa na Samia na pia zimefanyika juhudi katika uongozi wa Rais Samia katika mazungumzo ya kutafuta maridhiano na kuachiwa kwa wanasiasa na vyombo vya sheria isipokuwa wale ambao kesi zao ni za jinai zaidi.

Pamoja na kuondolewa kwa zuio la mikutano ya hadhara ya kisiasa, haya ni mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa sambamba na wanasiasa kutumia lugha zenye staha kwenye majukwaa.

Ilielezwa pia kwamba kama ilivyo nchi zilizoendelea kwenye demokrasia kama Marekani, baada ya uchaguzi, siasa zinahamia bungeni na kuwaacha wananchi wafanye kazi. Hilo ni jambo pia linalopaswa kuendelea kutufikirisha.

Kuondolewa kwa zuio la mikutano ya kisiasa kunaweka mazingira mazuri ya kuufanya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mwaka huu 2024 na ule mkuu wa mwakani 2025 kuwa chaguzi huru na wa haki kwani vyama vyote (tawala na upinzani) vimepewa fursa sawa za kunadi sera zao kwa wananchi, na yule mwenye hoja zenye mashiko, zinazogusa maisha ya wananchi basi atapata fursa ya kuongoza na kuwatumikia wananchi kupitia sanduku la kura.

Mara kadhaa, Rais Samia amesema yeye ni muumini wa kukosolewa, hivyo vyama vya upinzani viikosoe serikali kikamilifu kwa kutumia lugha za staha na kwa kuheshimu mila, desturi, sheria, kanuni na miongozo ya nchi yetu kwani kukosolewa kunaipa serikali nafasi ya kujua changamoto zilizopo kwa ajili ya kufanyia kazi.

Katika hafla hiyo na viongozi wa vyama vya upinzani, Rais Samia alisema, "Wajibu wenu ni kufuata sheria zinavyosema, ni kufuata kanuni zinavyosema ndiyo wajibu wenu. Lakini kama waungwana wastarabu niwaombe sana, tunatoa ruhusa ya vyama vya siasa twendeni tukafanye siasa za kistaarabu, za kupevuka. Tukafanye siasa za kujenga na si kubomoa, kurudi nyuma."

Saasa vyama vya siasa vimepata uwanja sawa wa kufanya siasa za ushindani kwa kutekeleza kwa vitendo haki ya kuandamana ili kufikisha ujumbe mbalimbali. Mathalani, chama kikuu cha upinzani, Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimefanya maandamano katika miji mbalibali kama vile Dar es Salaam, Arusha na Mwanza na kinaendelea na mipango ya kufanya maandamano katika miji mingine ili kufikisha ujumbe kwa serikali, huku jeshi la polisi likiilinda mikutano hiyo kikamilifu.

Vilevile, uhuru wa kujieleza kwa wananchi na kwa wanasiasa kwa ujumla ni nyenzo muhimu katika uwanja wa siasa. Uhuru wa kujieleza na kukosoa umepewa msukumo mkubwa na serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia kwani ni katika kujieleza na kukosoa kistaarabu na kiungwana, ndiko kunapotoka mawazo mazuri ya kujenga nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Wananchi wa aina zote waliosoma na wasiosoma, wanayo mawazo mazuri ambayo kama yakisikika na kufanyiwa kazi, yatachangia maendeleo ya nchi kwa kiasi kikubwa sana. Wanachama na viongozi wa vyama vya siasa nchini, wamehakikishiwa milango iko wazi wakati na muda wowote kushauri na kutoa maoni na mawazo yao ili serikali iweze kufanyia kazi kwa manufaa ya nchi.

Pia, Rais Samia amejitahidi sana kuweka mazingira wezeshi ya siasa za ushindani kupitia falsafa yake ya R4 yaani maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya. Wanasiasa wanapokuwa wameridhiana kwa pamoja na kuondoa vikwazo vilivyokuwa vikiathiri mshikamano na umoja wao, ni dhahiri siasa za ushindani zitafanyika vyema.



Rais Samia mara kadhaa amefanya vikao na viongozi wa vyama vya siasa ili kujenga maridhiano, huku ustahimilivu ukihitajika sana katika kusubiria hoja zinazotolewa kufanyiwa kazi na serikali.

Mageuzi katika sheria mbalimbali yamefanyika ili kufanikisha azma ya serikali kujenga upya nchi ili kufikia maendeleo endelevu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Lakini pia niwaguse wanasiasa, hususani wa upinzani kutumia haki yao ya kuzungumza kwa kuleta sera mbadala na suluhisho la matatizo yetu. Mfano, wanapolalamikia ugumu wa maisha au upungufu wa sukari, waeleze pia suluhusho la hilo.

Lakini pia watumie lugha zenye heshima na staha hasa wanapokuwa wanataja majina ya viongozi wetu wakuu. Kama kuna makosa, wawe na ushahidi huku wakitilia maanani kwamba hawa viongozi wetu ni binadamu wenye mapungufu, si malaika.

Kwa mafundisho ya Uislamu, Mtume Muhammad (SAW), aliwahi kuwaambia maswahaba zake kwamba kiongozi yeyote wa umma hasemwi kwa maneno yenye kukera mbele ya anaowaongoza hata akiwa ni dhalimu na kinachosemwa ni kweli bali hunasihiwa kwa maneno yenye staha. Mtume akafundisha kwamba hata baba ni kiongozi wa familia, ukienda kumdhalilisha mbele ya familia yake hata kama wewe ndiye mwenye haki, basi wewe ndiye unakuwa kwenye makosa.

Nihitimishe makala haya, kwa kukutakia afya nyema Rais Samia katika safari yako ya kuwatumikia wananchi ambao wana imani kubwa na wewe kuwa utasaidia kutatua kero zao na pia utasaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao ili wazidi kufurahia uongozi wako unaojali maisha ya wananchi wa aina zote.

Mungu ibariki Tanzania na watu wake wote.

> KIMSINGI, tangu Rais Samia aingie madarakani, amefanya mengi mazuri huku akigusa nyanja zote za maisha yaani kijamii, kiuchumi na kisiasa.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma: Maoni: 0620 800 462.***



# Fikra za Nyerere katika kilimo ziko hai utawala wa Samia



**Na Hamisi Kibari**

MWALIMU Julius Nyerere aliamini maendeleo yataletwa kwa kutilia maanani vitu vinne; raslimali ardhi, raslimali watu, siasa safi na uongozi bora.

Bila shaka, hadi leo umuhimu wa mambo hayo manne katika kusukuma maendeleo ya nchi yetu uko palepale. Kwenye ardhi ambayo tumejaaliwa na Mungu kuwa nayo ya kutosha, yapo mengi ambayo tunapaswa kuifanyia na kutuhakikishia maendeleo, kubwa likiwa ni kilimo.

Ni katika muktadha huo, mwaka 1972, Serikali ya Mwalimu Nyerere ilitangaza Azimio la Iringa lililokuwa na kaulimbiu ya 'Siasa ni Kilimo', likijielekeza katika kutumia vizuri nguvu kazi ya watu ili kuleta mapinduzi ya kilimo.

Azimio hili lilieleza kwamba ni muhimu kilimo kitosheleze mahitaji yafuatayo: kwanza, kuwapatia wakulima chakula chao wenyewe; pili, kuwalisha watu wengine wote (mfano wafanyakazi na wafanyabiashara); tatu, kuipatia nchi fedha za kigeni; nne, kutoa malighafi za viwandani na tano, kutoa ajira.

Mwalimu Nyerere pia alikuja na falsafa ya 'Kilimo cha Kufa na Kupona' iliyolenga kupambana na njaa iliyoikumba dunia miaka ya 1970.

Mwalimu aliona pia umuhimu wa siasa kutambua na kuzingatia mbinu za kisasa ili kukuza kilimo nchini, hatua ambayo ingesaidia pia kupunguza wimbi la vijana kuhamia mijini.

Halikadhalika, Mwalimu alitaka Tanzania ifanye vyema zaidi katika soko la bidhaa za kilimo na kukuza viwanda na kwa mantiki hiyo akaanzisha vituo vya utafiti wa mazao ya chakula na mazao ya biashara kama Uyole (Mbeya), Tengeru (Arusha), TPRI (Arusha) na vinginevyo.

Miaka takribani 24 baada ya Mwalimu Nyerere kuondoka duniani, bado kilimo kina dhima ileile ya kuitosheleza Tanzania katika mahitaji hayo matano.

Karibu viongozi wote baada ya Mwalimu Nyerere wameendeleza mtazamo huo wa kukuza kilimo chetu ili kitoe manufaa makubwa zaidi. Serikali ya awamu ya nne, kwa mfano, ilikuja na falsafa ya 'Kilimo Kwanza' iliyolenga kuimarisha ushirikiano wa serikali na sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza kilimo.

Kwa upande wake, Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita, Dk. Samia Suluhu Hassan, amefanya mengi katika kilimo licha ya kupokea kijiti cha uongozi katika kipindi ambacho uchumi wa dunia ulikuwa umetikiswa na janga la Uviko-19 na kufuatiwa na vita baina ya Urusi na Ukraine.

Baadhi ya mambo yaliyofanywa na serikali yake ni kuongezea bajeti katika kilimo, kuboresha utendaji wa maofisa ugani, kuanzisha mfumo wa utoaji ruzuku ya mbolea, kuanzisha miradi zaidi ya 20 ya kilimo cha umwagiliaji na kuanzisha programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT).

Yapo mengi ya kuchambua kuhusu namna Rais Samia anavyouenzi mtazamo wa Mwalimu Nyerere katika kukuza kilimo, lakini makala haya yanajikita zaidi katika kuangalia manufaa ya programu ya BBT iliyozunduliwa wakati wa Maonesho ya Nanenane, Agosti 3 mwaka juzi jijini Mbeya.

BBT ni mkakati maalumu unaolenga kuwaunganisha vijana, wakiwemo wasomi na walioko kwenye makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kufanya shughuli za kilimo na ufugaji wa kisasa na wenye tija.

Katika programu hii, serikali kwa kushirikiana na wadau wake mbalimbali inaweka mazingira mazuri kwa kuanzisha miradi ya mashamba makubwa ambayo vijana wanapewa maeneo na hati za kuyamiliki.

Tayari serikali ya Dk. Samia imeshazungumza na benki mbalimbali ambazo zitawapatia mikopo kwa msharti nafuu huku na yenyewe ikitenga mabilioni ya pesa kwa ajili hiyo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa anasema: "Vijana msiwe na hofu ya kupata mitaji kwa ajili ya kilimo kwa sababu serikali imetoa maelekezo kwenye mabenki yote kukopesha wajasiriamali wakiwemo vijana wanaojishughulisha na kilimo."

Kupitia mpango huo unaotarajia kuajiri vijana milioni moja ifikapo mwaka 2025, vijana wanapatiwa elimu ya kilimo au ufugaji wa kisasa kabla ya kuanza jukumu hilo.

Wakishazalisha serikali pia inawasaidia kupata masoko ya ndani na nje. Katika muktadha huo, Rais Samia amekuwa akisema safari zake nje zimemsaidia pia katika kupata masoko ya mazao ya Tanzania, hivyo ni vijana tu washindwe wenyewe!

Wakizungumzia programu hiyo, maofisa waandamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) wanasema mpango wa BBT na mingine ikiwemo ya kuongeza bajeti katika kilimo, inaonesha kuna utashi mkubwa wa kisiasa utakaoharakisha mapinduzi ya kijani nchini.

Mmoja wa watafiti waandamizi wa TARI, Dk Joel Meliyo, alisema haya muda mfupi baada ya BBT kuzinduliwa mwaka jana: "Kwa hakika utashi wa kisiasa ni injini ya mambo mengine kuweza kutokea. Kama kuna utashi, hakuna kinachoshindikana. Kutokana na utashi wa kisiasa, ndio maana watu wanafika mwezini."

Anasema kwa sasa vijana wengi wanaonekana hawana mwamko mkubwa, lakini kilimo kinahitaji uwekezaji wa kutosha na hivyo hatua hii ya serikali ni mwarubaini wa kuwavuta vijana ambao ndio injini ya maendeleo ya nchi.

"Vijana wanahitaji kuandaliwa vizuri ili wajue wanalima nini na mtaji watapata wapi, watauza wapi na hayo yote inaonekana yatawezekana kwa kuwa kuna utashi wa kisiasa," anasema.

Akizungumza mwaka juzi na mwandishi wa makala haya baada ya BBT kuzinduliwa, Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano cha Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Neema Sitta, alipongeza kwa dhati mpango huo.

Alisema vijana wengi wanaomaliza shule na vyuo hawana ardhi kwani bado ardhi inamilikiwa na wazee wao, hivyo hatua ya serikali kuja na mkakati wa kuwapatia ardhi ni wa kupongezwa sana kwani "nchi bado ina ardhi ya kutosha."

"Kingine ni matumizi ya teknolojia katika kilimo. Vijana wa sasa huwezi kutegemea wavutike kulima kwa jembe la mkono na hivyo serikali imekuwa na ufumbuzi muhimu sana wa kuwawezesha mitaji kwa kuwaunganisha na benki ili walime kwa kutumia teknolojia," anasema.

Mmoja wa viongozi wa Bodi ya Korosho Tanzania, Francis Alfred anasema hatua ya kuwavuta vijana kwenye kilimo ni suluhisho la ajira na maisha bora kwa Watanzania.

Anasema Bodi ya Korosho ilishaliona hilo mapema na hivyo kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya korosho (block farming) ambamo vijana wanagawiwa maeneo ya ekari tanotano.

Anasema kwenye mashamba hayo makubwa ni rahisi kuwanyanyua vijana kuliko wanapokuwa wakilima mmoja mmoja kwa kuwa mashamba makubwa yatakuwa na miundombinu muhimu na rahisi pia kupeleka utalaamu.

Anasema kupitia mashamba hayo ni rahisi pia kuweka viwanda vya kuongeza thamani ya mazao, hatua inayowahakikishia soko.

Hata hivyo, vijana wanapoingia kwenye kilimo wanahimizwa wasifikirie kupata pesa za harakaharaka kwani inaweza kuwachukua muda. Wataalamu wa TARI wanasema kama mkakati ukienda ulivyo, nchi inakwenda kuzalisha mabilionea lukuki kupitia kilimo miaka michache ijayo.

Vijana pia wanatakiwa kuondoa mtazamo finyu wa kwamba akimaliza kozi yake, apate kazi ya ofisini, apange chumba na kuingia kazini kuanzia saa mbili asubuhi na kutoka saa 11.

Ni kwa kulijua hilo, maofisa wa TARI wanasema vijana watakaochangamkia programu ya BBT wanaweza kupiga hatua kubwa sana kuliko wenzao wanaosubiri ajira.

Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba tayari mpango huo umeshaandikisha zaidi ya vijana 7,000.

Rais Samia alipotembelea Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nanenane) jijini Mbeya Agosti 8 mwaka jana alipongeza juhudi zilizokwisha chukuliwa.

Akiwa kwenye mabanda ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Samia alipongeza hatua ya programu ya BBT – LIFE katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kuwapatia vijana mafunzo ya vitendo ya unenepeshaji wa ng'ombe, kaa, jongoo bahari, pamoja na kilimo cha mwani.

Alisema soko la nyama nje ya nchi ni kubwa hivyo kupitia programu ya BBT – Life vijana wanaopatiwa mafunzo ya kunenepesha ng'ombe wanapaswa kutumia fursa hiyo ili kunenepesha ng'ombe kwa wingi.

Baadhi ya vijana wanaonufaika na BBT – Life walimshukuru Rais Samia kwa kuanzisha programu hiyo ambayo ina manufaa makubwa kwao kwa kuwa inawaongezea maarifa na kuwahakikishia kipato.

Tunapoadhimisha leo miaka mitatu ya uongozi wake, tuendelee kumuunga mkono Rais Samia na serikali yake kwa kuonesha siasa safi na uongozi bora katika kuboresha kilimo.




Rais Samia Suluhu Hassan akizinduwa Masafa ya 5G

# Upeo na maono imara kidijitali

Na Mwandishi Wetu

MAKALA hii inachambua mafanikio ya Sekta ya Mawasiliano Tanzania, ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan (Machi 2021–Machi 2024)

**UTANGULIZI**

KUENEA kwa miundombinu mipya ya mawasiliano, kuongezeka kwa watoa huduma na watumiaji wa huduma za mawasiliano na Tanzania kujiimarisha kimataifa vinathibitisha upeo na maono imara ya Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuimarisha sekta ya mawasiliano nchini kama mwezeshaji mkuu wa uchumi wa kidijitali.

Miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais Dk. Samia imeshuhudia Tanzania ikipata nafasi anga za juu kwa ajili ya satelaiti yake na mkongo wa nne wa kimataifa wa mawasiliano ya kasi ukiingia Tanzania. Vilevile ugawaji wa masafa ya intaneti ya kasi umefanyika, nchi imekuwa kitovu cha mawasiliano ya posta Afrika na imerudisha nafasi yake kwenye vikao vya Taasisi za Mawasiliano za Kimataifa.

Yote haya yamekuja wakati viashiria muhimu vya ukuaji wa sekta vikionesha kupanda kwa asilimia ya kuenea huduma za mawasiliano kijiografia na kuongezeka matumizi yake miongoni mwa watumiaji kati ya Machi 2021 na Machi 2024.

Ni kipindi ambacho Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ya Mapinduzi Zanzibar zinatekeleza mipango ya kujenga uchumi wa kidijitali na wa buluu. Uchumi wa Kidijitali ni ule ambao nchi inajenga mwelekeo tawala wa

Inaendelea Uk. 13

Inatoka Uk. 12

| Jedwali 1: Kuenea kwa teknolojia ya mawasiliano Desemba 2020, Desemba 2021, Desemba 2022 na Desemba 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Na. | Maelezo | Mwaka/Asilimia | | | |
| | | Desemba, 2020 | Desemba, 2021 | Desemba, 2022 | Desemba, 2023 |
| 1. | Kuenea uzao wa pili (2G) miongoni mwa watu | 94% | 95% | 95% | 96% |
| 2. | Kuenea uzao wa tatu (3G) miongoni mwa watu | 59% | 63% | 72% | 86% |
| 3. | Kuenea uzao wa nne (4G) miongoni mwa watu | 33% | 47% | 55% | 79% |
| 4. | Kuenea kijiografia | 63% | 65% | 66% | 73% |
| 5. | Kuenea simu zenye uwezo mkubwa (simu-janja) | | | 25% | 32.12% |

| Jedwali 2: Mwelekeo wa wa usajili laini za simu za mkononi na akaunti za pesa kwa simu: Desemba 2021 hadi Desemba 2023. | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | Akaunti | Ongezeko | Asilimia ya ongezeko (%) | Laini za simu | Ongezeko | Asilimia ya ongezeko (%) |
| Desemba 2021 | 35,285,767 | 3,017,137 | 9.35 | 54,044,384 | 2,824,151 | 5.51 |
| Desemba 2022 | 40,953,496 | 5,667,729 | 16.06 | 60,192,331 | 6,147,947 | 11.37 |
| Desemba 2023 | 52,875,129 | 11,921,633 | 29.1 | 70,215,144 | 10,023,034 | 16.65 |
| Wastani wa asilimia ya ongezeko | | | 18.17 | | | 11.17 |

| Jedwali 3: Mwelekeo wa wastani wa gharama za upigaji simu, kutuma meseji na kutumia data kupitia kifurushi (bando) - kwa shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023 |
| Ndani ya Mtandao | 7.8 | 7.3 | 4.9 |
| Nje ya Mtandao | 8.7 | 7.8 | 6.3 |
| Meseji | 3.3 | 2.7 | 2.1 |
| Data | 1.6 | 1.9 | 2.1 |

| Jedwali 4: Mwelekeo wa akaunti za pesa kwa simu, idadi ya miamala kati ya 2021 na 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 |
| Akaunti za pesa kwa simu | 35,285,767 | 40,953,496 | 52,875,129 |
| Idadi ya miamala | 3,752,084,894 | 4,195,899,414 | 5,273,086,154 |
| Chanzo: Tovuti ya TCRA: https://www.tcra.go.tz/communications/statistics.pdf | | | |

| Jedwali 8: Mwelekeo wa vitu vilivyotumwa nje ya Tanzania kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023. | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Maelezo/Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 | Asilimia ya ongezeko (%) |
| Vitu vilivyotumwa kwenda nje ya Tanzania | 564,528 | 937,124 | 979,625 | 73.52 |

matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na mifumo ya kielektroniki kwenye sekta zote. Uchumi wa Buluu ni pale nchi inapoweka mkazo kwenye matumizi ya rasilimali na fursa zinazotokana na bahari au fukwe kujiendeleza kiuchumi.

**TEKNOLOJIA YA 5G**

Upangaji na usimamizi mzuri wa rasilimali za mawasiliano (masafa na namba), ndio unaowezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano pamoja na huduma za pesa mtandao. TCRA imefanikiwa kugawa masafa yanayowezesha utoaji wa huduma ya intaneti ya kasi. Jitihada hizi zitawezesha wananchi wengi kupata huduma za intaneti ya kasi ambayo ni muhimu sana wakati huu tukiwa kwenye uchumi wa kidijiti. Malengo ya Serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2025 asilimia 80 ya wananchi wanapata huduma ya intaneti ya kasi.

TCRA pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kiusimamizi imetoa rasilimali masafa katika bendi za 700MHz, 2300MHz, 2600MHz na 3500MHz yanayowezesha intaneti ya kasi ya 4G na 5G. Kuwepo kwa intaneti ya kasi kunawezesha uchumi wa kidijiti katika maeneo mbalimbali kama vile huduma za kifedha, utalii, viwandani, kilimo na huduma za afya. Aidha, TCRA ipo katika hatua za awali za kufungua bendi za masafa ambazo zitatumiwa na watoa huduma bure bila kuhitaji kuwa na leseni ya rasilimali masafa (Unlicensed bands), hatua hii itaongeza matumizi ya intaneti kwa kuwa na huduma za intaneti za wazi (WiFi -hotspots).

**MABORESHO YA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO**

Uwepo wa Mkongo wa Taifa na ongezeko la minara vimepelekea mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano ya simu za mkononi imeendelea kutoka uzao wa kwanza unaojulikana kama 1G ambao ulikuwa wa maongezi (sauti) tu na wa analojia kwenda uzao wa pili (2G), wa tatu (3G), wa nne (4G) na sasa wa tano (5G). Hadi Desemba 2023, simu za uzao wa pili (2G) zilifikia asilimia 98 ya watu nchini (kutoka asilimia 95 mwaka 2022), uzao wa tatu (3G) umefikia asilimia 86 kutoka asilimia 72 na uzao wa nne (4G) asilimia 79 kutoka 55.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri K. Bakari amesema kwenye taarifa ya Mamlaka ya robo mwaka ya Oktoba hadi Desemba 2023 kwamba taasisi yake itafuatilia kwa kina gharama za simu janja, kwani kutokuenea kwa simu janja kwa watumiaji wengi ni mojawapo ya sababu za kutokuenea kwa matumizi ya intaneti kwa kasi.

"Uwiano kati ya mitandao na matumizi ya intaneti unaonesha kuwa maeneo mengi yamefikiwa na huduma za intaneti ila kuna watumiaji wachache; sababu ikiendelea kuwa ni idadi ndogo ya watumiaji wenye simu janja," amesema.

Simu hizi ni muhimu katika kuendeleza matumizi ya intaneti, kwani takwimu za mawasiliano za Desemba 2023 zinaonesha kuwa laini za simu 35,885,592 zilitumika kupata huduma ya intaneti. Asilimia 99.8 ya watumiaji wa intaneti wanatumia simu na vifaa vya mkononi, zikiwemo tableti.

Miundombinu pia imejengwa na huduma kufikishwa Kijiji cha Msomera, wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga, ambako waliokuwa wakazi wa Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCAA) wamehamia kwa hiyari na wamepangiwa makazi. Pia TCRA imejenga kituo cha TEHAMA (Telecentre) kwa ajili ya Shule ya Sekondari Msomera na jamii inayoizunguka.

Miundombinu inayowezesha mawasiliano ya kasi kimataifa imeendelea kuimarishwa, ambapo Agosti 2023, Mkongo wa Nne wa Kimataifa wa Faiba (2Afrika) unaopita baharini uliingia Tanzania kipindi ambacho nchi inajizatiti kidijitali. Utaunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ya Kasi (NICTBB) ambao umefika mipakani mwa nchi zinazopakana na Tanzania, ambazo baadhi zinautumia.

**UFIKIWAJI WA MAWASILIANO TANZANIA BARA NA ZANZIBAR**

Katika jitihada za kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora za mawasiliano, TCRA kwa kushirikiana na UCSAF imeleta mapinduzi makubwa kwenye ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya mawasiliano mathalani ujenzi wa minara 42, katika shehia 38 Unguja na Pemba ulianza Novemba 2022, mradi huu unatarajiwa kutatua changamoto ya mawasiliano ya simu kwa wananchi wa visiwa vya Pemba na Unguja. Huduma zitakazowezeshwa na minara hii zitanufaisha wananchi 211,601 ambapo minara sita inajengwa Mkoa wa Kaskazini Pemba, saba Kusini Pemba, 12 Kaskazini Unguja, 10 Unguja Kusini na saba Mjini Magharibi.

Jijini Dodoma, Mei 2023 mikataba ilisainiwa kwa ujenzi wa minara 758 katika kata 713 na kuongeza uwezo na nguvu ya minara 304 katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara ambayo yana mawasiliano hafifu. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18 kuanzia mikataba iliposainiwa; yaani ifikapo Disemba 2024. Hii itawezesha zaidi ya Watanzania milioni tatu kupata huduma za intaneti kwa mara ya kwanza na laini zaidi ya milioni sabini kutumika kwenye mitandao ya simu.

Lengo la ujenzi huu ni kuongeza nguvu ya minara kutoka teknolojia ya uzao wa pili, yaani 2G kwenda teknolojia za juu zaidi hadi kufikia uzao wa tano (5G). Uzao huu unawezesha maongezi, meseji, data, video, picha na matumizi makubwa ya mtandao wa mambo (IoT).

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape M. Nnauye (Mb) amesema uwekezaji huu utachangia uchumi wa nchi, kazi ambayo pia ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inayolenga pamoja na mambo mengine, kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanapata huduma bora zaidi za intaneti ifikapo Oktoba 2025.

Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti (Laini za Simu, Akaunti za Pesa na Miamala ya Pesa)

Vidokezi vya ukuaji wa sekta vinaonesha mabadiliko ya kasi kwenye maeneo mengi. Kwa mfano, kasi ya usajili wa akaunti za pesa kwa simu za mkononi

Inaendelea Uk. 14

# MIAKA MITATU YA DK. SAMIA



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika hali ya bashasha ndani ya Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ghorofa ya kumi na mbili (12) alipozinduwa Makao Makuu ya Umoja wa Posta, Barani Afrika (PAPU Towers) jijini Arusha. Pamoja na Rais ni Waziri wa Habari Mawasiliano na teknolojia ya Habari. Nape Moses Nnauye na Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dr. Jabiri K. Bakari.**

Inatoka Uk. 13

ulizidi ile ya usajili wa laini za simu kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023. Hii inaashiria kwamba watumiaji wengi wa simu za mkononi wanajisajili kwa huduma za fedha mtandaoni na kidijitali.

Wakati usajili wa laini za simu uliongezeka kwa wastani wa asilimia 11.17 kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023, usajili wa akaunti za fedha kidijitali uliongezeka kwa wastani wa asilimia 18.17.

Laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka 54,044,384 ambazo zilienea kwa asilimia 91 miongoni mwa Watanzania Desemba 2021 hadi 70,292,899 zilizoenea kwa asilimia 111 Disemba 2023 kutokana na unafuu na urahisi wa upatakanaji wa huduma

Miamala ya kifedha kupitia simu za mkononi Tanzania imeongezeka kwa asilimia 30 kati ya Septemba na Desemba 2023 na kwa asilimia 44 ndani ya mwaka mmoja, hali inayoakisi kukua mfumo jumuishi wa kifedha nchini.

Akaunti za pesa kwa simu zimeongezeka kutoka 51,369,347 ambazo zilifanya miamala 422,390,546 Septemba 2023 na kufikia 52,875,129 zilizofanya miamala 549,529,470 Desemba mwaka huo.

Huduma za fedha mtandao zimezalisha ajira nyingi, zikiwemo za wakala. Vilevile benki nyingi zimeboresha na kurahisisha huduma zake ambapo zinawatumia watoa huduma hawa kama wakala wao ili kufikisha huduma za kibenki karibu na wateja wao.

Pamoja na kuleta ufanisi, huduma za fedha kupitia simu za mkononi pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi, hasa baada ya serikali kuanzisha Mfumo wa Malipo ya Kiserikali Mtandaoni (GePG).

TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za simu za mkononi na kuwapa namba za mawasiliano na misimbo, au namba fupi ya kuwezesha miamala hiyo. Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inasimamia sekta ya fedha kwa ujumla na inatoa leseni za huduma za fedha mitandaoni. Taasisi hizi zinashirikiana kwenye masuala ya fedha mtandaoni.

Huduma za pesa kwa simu za mkononi zimefungua fursa kwa watu wengi. Usajili wa laini za simu kibiometria unawapatia Watanzania utambulisho wa kipekee kidijitali na pia umeongeza imani ya watumiaji kwenye miamala na huduma za kielektroni.

Pamoja na kukua kwa huduma za pesa mtandao, gharama za mawasiliano zimeshuka ndani ya miaka mitatu iliyopita. Hizi ni pamoja na gharama za kupiga simu nchi za Afrika Mashariki.

Takwimu za Desemba 2023 zinaonesha kuwa dakika za simu za kimataifa zinazoingia nchini zimeongezeka kwa asilimia 29.2; kutoka 2,216,904 Septemba 2023 hadi 3,129,711 Desemba 2023.

## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA POSTA

Masuala mengi yaliyoshughulikiwa ndani ya miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais Dk. Samia ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kuifanya Tanzania kuwa ya kidijitali. Mradi wa Tanzania ya kidijitali unakusudia kujenga mwelekeo tawala wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kuendesha shughuli za serikali, huduma za jamii na za kiuchumi.

Mradi huo unahusisha pia uimarishaji wa miundombinu ya mawasiliano katika miji ili kuifanya iwe ya kisasa. Kwa kuanzia majiji ya Dodoma, Arusha na Mbeya yatafanywa ya kidijitali, hivyo kuyawezesha kuungana na majiji maarufu barani Afrika kama vile Cape Town, Afrika Kusini ambayo yana hadhi hiyo.

Sifa moja wapo ya jiji la kisasa ni kuwepo kwa mifumo ya kielektroniki inayosimamia huduma za umma na za kiusalama ikiwa ni pamoja na kuwezesha taa za kuongoza magari, kubaini mwelekeo wa foleni, mfumo wa kielektroniki wa kukusanya data za matumizi ya umeme, maji na huduma za taka. Uboreshaji maisha ya wakazi kupitia matumizi ya TEHAMA na ufanisi wa huduma yanatawala shughuli zote za

Inaendelea Uk. 15

Inatoka Uk. 14

| Leseni za huduma za mawasiliano ya simu, intaneti, utangazaji na posta kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina/Mwaka** | **2021** | **2022** | **2023** |
| Kujenga na kuendes;ha miundombinu | 29 | 31 | 36 |
| Kutumia miundombinu kutoa huduma mbalimbali | 16 | 17 | 17 |
| Huduma tumizi za mawasiliano | 105 | 120 | 146 |
| Televisheni za maudhui yasiyolipiwa | 36 | 36 | 41 |
| Vituo vya redio | 201 | 220 | 237 |
| Huduma za posta ya umma | 1 | 1 | 1 |
| Usafirishaji vifurushi | 135 | 78 | 117 |
| Kimataifa | 4 | 5 | 6 |
| Afrika Mashariki | 3 | 1 | 1 |
| Ndani ya Tanzania | 31 | 48 | 59 |
| Kati ya miji | 40 | 54 | 70 |
| Ndani ya mji | 9 | 13 | 18 |

majiji hayo.

Kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Dk. Samia pia kimeshuhudia Tanzania ikijiimarisha kama Kitovu cha Mawasiliano ya Posta Afrika kufuatia kufunguliwa kwa Kituo cha Kimataifa cha Teknolojia ya Sekta hiyo na ofisi ya kanda ya Umoja wa Posta Ulimwenguni (UPU) Jijini Arusha lililofunguliwa na Rais Dk. Samia, Septemba 2023. Kituo hicho na ofisi hiyo vitakuwa kwenye jengo la kisasa la Umoja wa Posta Afrika (PAPU), ambalo limejengwa kwa ubia wa serikali ya Tanzania na Umoja huo.

Tanzania imeweka miundombinu muhimu ya huduma za posta zinazowezeshwa na ubunifu, ikiwa ni pamoja na mfumo wa anwani za makazi na postikodi ambao unatarajiwa kuwezesha ufikishaji na uchukuaji vitu vinavyonunuliwa mitandaoni na kuhitajika kufikishwa kwenye makazi au ofisi za wahusika.

Shirika la Posta Tanzania (TPC) limeonesha ongezeko la vitu lilivyosafirisha kwenda nje ya Tanzania kati ya 2021 na 2023. Hata hivyo, idadi ya vitu vilivyosafirishwa ndani ya nchi vimeendelea kupungua. Sababu mojawapo ni kuwa ni ushindani unaotokana na kuongezeka kwa watoa huduma za kusafirisha vifurushi ndani ya nchi na kati ya miji. (rejea jedwali 9).

## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA UTANGAZAJI

Vilevile jambo lingine la kusisimua kwa namna yake mwaka 2023 ni Tanzania kupata nafasi katika obiti ya satelaiti kwa ajili ya satelaiti ya utangazaji; mafanikio yatakayowezesha kuenea huduma za utangazaji hasa kwenye maeneo yasiyo na usikivu mzuri wa redio yaliyopo pembezoni mwa nchi na yaliyozungukwa na milima ambapo matangazo ya mfumo wa utangazaji wa FM hayafiki.



Maafisa wa TCRA wakufuatilia Masafa  kwakutumia kifaa cha jongefu cha mkononi.

Mipango ya kufikisha huduma za mawasiliano sehemu zote nchini, ikiwa ni pamoja na kutumia satelaiti na ujenzi wa miundombinu mipya.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dk. Jabiri K. Bakari ameeleza kuwa mikakati imekamilika kutatua changamoto ya huduma za utangazaji wa redio kutofika baadhi ya sehemu zenye mazingira magumu kijiografia, hasa zilizo pembezoni na maeneo yenye milima na mabonde. Mfano ni maeneo ya Rombo mkoani Kilimanjaro.

Katika dhamira ya kuboresha na kuleta ufanisi katika Sekta ya Utangazaji, Serikali kupitia TCRA imepunguza ada kadhaa za leseni  na kuboresha miongozo na taratibu za utangazaji kuhakikisha wananchi wanapata wigo mpana zaidi wa kuchagua kituo gani cha kusikiliza au  aina ya maudhui.

Ushirikishwaji wa wadau katika kuboresha Sekta ya Mawasiliano ya Kielektoniki na Posta

TCRA imeendelea kukutana na kushirikiana na wadau wa Sekta ya Mawasiliano ambapo maoni yao yamepelekea maboresho ya Kanuni za Leseni za Huduma za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta mwaka 2022. Hatua hii, imeongeza fursa kwa wajasiriamali kwenye sekta ndogo za Posta na Utangazaji na kwenye utoaji huduma kupitia mitandao ya mawasiliano ya simu.  Kanuni zimeanzisha aina mpya ya leseni zinazowezesha kutoa huduma za biashara mtandao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Bakari ameeleza kwamba jamii iliyojipanga vizuri na inayojishughulisha inaweza kujenga uchumi shirikishi kupitia mifumo ya mawasiliano ya simu na intaneti ya ubora wa juu, inayoaminika, nafuu na inayopatikana sehemu nyingi.

## JITIHADA ZA KUCHOCHEA BUNIFU ZA TEHAMA

TCRA pia imeanzisha utaratibu wa kutoa bure raslimali za mawasiliano kwa wabunifu ili kufanya majaribio ya uvumbuzi wao utakaofaidisha jamii. Lengo ni kujenga ujasiriamali na kupanua wigo wa huduma za mawasiliano. Raslimali hizi ni pamoja na masafa, namba, misimbo, na Kikoa cha Taifa (.tz) - yaani jina mahsusi linalotambua raslimali za intaneti kama vile tovuti zilizosajiliwa nchini na ngazi nyingine duniani.

## KLABU ZA KIDIJITI

Katika kuendelea kuchagiza na kuandaa Tanzania kwenye uchumi wa kidijiti mwaka 2022 TCRA kwa kushirikiana na wizara ya habari, teknolojia ya habari na mawasiliano ilianzisha klabu za kidijiti kuanzia shule za awali mpaka vyuo vikuu, kwa lengo la kukuza uelewa wa (TEHAMA), ubunifu na kuhakikisha sekta ya mawasiliano inachagiza ukuaji wa pato la taifa, katika kuboresha klabu hizi mwaka 2023 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imezindua kitabu cha Kuanzisha na Kuratibu klabu hizi.

## KIKOA CHA TAIFA (.TZ)

TCRA imeendelea kusimamia na kuendesha rajisi ya majina ya kikoa cha taifa cha .tz. Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2023 usajili wa kikoa cha .tz umefikia 29,006. Lakini pia



Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhiwa Kishikwambi alipozinduwa Ujenzi wa Minara zaidi ya miasaba  ya Mawasiliano  vijijini. Shughuli hiyo ilifanyika Dodoma.

Inaendelea Uk. 16

## MIAKA MITATU YA DK. SAMIA




Mitambo jongefu waufuatiliaji Masafa.

**Inatoka Uk. 15**

TCRA imeimarisha usalama wa vikoa kwa kuongeza viendelezi vya usalama wa mfumo wa majina ya vikoa (DNSSEC) hii ikijumuisha takribani vikoa vyote vya serikali (.go.tz). Pia, imeithinisha vyeti vya ithibati kwa wasajili wa vikao kufikia idadi ya wasajili 79. Kikoa cha Taifa ni utambuzi rasmi wa Tanzania katika mtandao kama namba +255 kwenye simu.

TCRA inaendelea kuhakikisha uwepo wa rasilimali zinazowezewesha mawasiliano ya intaneti. Usimamizi wa rasilimali hizi umeweza kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Utoaji leseni na Vyeti vya Ithibati (Tanzanite Portal)

TCRA imeongeza ufanisi katika kuhudumia mteja kupitia dirisha moja la maombi ya leseni za aina zote, utoaji wa vyeti vya uhakiki wa vifaa vya kielektroniki, anuani za makazi na dawati la huduma kuwezesha mawasilisho ya malalamiko ya wateja

TCRA imeendelea kutoa leseni na kusimamia masharti ya leseni kwa watoa huduma za mawasiliano nchini. Leseni za huduma kuu za mawasiliano ya simu, intaneti, maudhui ya utangazaji na posta na usafirishaji wa vifurushi zimeongezeka, hasa zile za programu tumizi za mawasiliano, ambazo zinawezesha matumizi ya intaneti

Mafanikio haya yametokana na uwepo sera imara, sheria nzuri na mifumo wezeshi ya kiusimamizi na utoaji leseni. TCRA imeendelea kuendeleza shughuli zake za usimamizi wa sekta ya mawasiliano nchini kwa kushirikisha wadau wa sekta katika maamuzi yote muhimu ya maboresho na ufanisi wa sekta. Ushirikishwaji huo umewezesha watoa huduma kuzingatia miongozo, kanuni na sheria za sekta, usimamizi shirikishi umeongeza idadi ya watoa huduma na ubora wa huduma.



Makao Makuu ya Umoja wa Posta, Barani Afrika (PAPU Towers), Arusha.


KAMATA
Gazeti lako kiganjani
Uelekeo

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA EPZ (EPZA)

# Maeneo muhimu yanayopaswa kujumuishwa katika Hotuba ya Bajeti itakayowasilishwa Bungeni Aprili, 2024

**1. UTANGULIZI**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), ni Taasisi ya Serikali inayofanya kazi zake chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

EPZA ilianzishwa mwaka 2006 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Programu ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (Export Processing Zones – EPZ) ya mwaka 2002, ili kusimamia utekelezaji wa programu ya EPZ.

Mwaka 2011, majukumu ya EPZA yaliongezwa na kuifanya isimamie mpango ambao ni mpana wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (Special Economic Zones – SEZ).

Hii ni kufuatia marekebisho ya Sheria za EPZ na SEZ ya mwaka 2011, yaliyofanya EPZ kuwa sehemu ya programu ya SEZ.

Malengo ya EPZA ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda kwa uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje ya nchi ili kuongeza pato la fedha za kigeni, kuongeza fursa za ajira, usindikaji wa malighafi za ndani na kuvutia teknolojia mpya.

Majukumu ya EPZA ni pamoja na kutwaa na kumiliki Maeneo Maalum ya Kiuchumi, kujenga miundombinu, kutoa leseni za uwekezaji za EPZ na SEZ, kuhudumia wawekezaji kabla na baada ya kupata leseni na kutangaza fursa za uwekezaji ndani ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi.

Program ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ), ilianzishwa kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ) ya mwaka 2002. Program hii inahamasisha uwekezaji wa viwanda vinavyouza nje ya nchi vilivyopo katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa lengo la kukuza ushindani wa kimataifa na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

Program ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (Special Economic Zones - SEZ) ilianzishwa kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya mwaka 2006. Programu hii inahamasisha uwekezaji kwenye sekta mbalimbali kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje ya nchi, ambapo program ya EPZ ni sehemu ya programu ya SEZ.

Utekelezaji wa program ya SEZ ulianza rasmi mwaka 2011 baada ya sheria za EPZ na SEZ kufanyiwa marekebisho na kanuni za SEZ kutungwa.

**2. MAFANIKIO YA EPZA TANGU KUANZISHWA KWAKE**

Taswira ya uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi tangu taasisi hii ianzishwe kwa mujibu wa viashiria vikuu vinavyotumiwa na Mamlaka ya EPZ imeonyesha kuwa na mafanikio makubwa ambapo jumla ya miradi 221 imesajiliwa na EPZA katika maeneo mbalimbali nchini kupitia leseni za EPZ na SEZ, miradi mingine ikiwa ndani ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi na mingine ikiwa imewekezwa katika maeneo binafsi ya wawekezaji (Standalone Factories).

Miradi hiyo imevutia jumla ya mtaji wa Dola za Marekani milioni 3,542.4 na kuongeza ukuaji wa mauzo ya nje yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2,212.4 na ajira zipatazo 70,000.

Aidha, miradi hiyo imejikita katika sekta zinazozalishwa bidhaa zitokanazo na kilimo (Agro Processing), bidhaa za mifugo, bidhaa za kemikali, bidhaa za madini, viwanda vya nguo na bidhaa za mazao ya misitu.

Mafanikio haya yamepatikana kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2007 taasisi hii ilivyoanza kusajili miradi hadi Februari, 2024 kutokana na mazingira mazuri ya biashara yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambapo pia ilihusika hata katika kuhamasisha uwekezaji nchini kwa njia mbalimbali.

**3. TAARIFA YA MAENDELEO YA MIRADI**

**a. Benjamin William Mkapa SEZ**

Hili ni Hifadhi ya Viwanda ya kwanza kuanzishwa na inayomilikiwa na Serikali. Hifadhi hii ya viwanda iko kimkakati katika eneo la Mabibo External, kando ya Barabara ya Nelson Mandela; Dar es Salaam. Hifadhi hii ina jumla ya eneo la ekari 65 ambapo viwanja vya viwanda na majengo ya viwanda, yanachukua asilimia 74 ya eneo hilo sawa na ekari 48.

Serikali kupitia EPZA, ilisimamia ujenzi wa miundombinu katika BWM-SEZ mwaka 2006.

Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na viwanja vya viwanda, majengo ya utawala, maduka, jengo la forodha, barabara, taa za barabarani, ukuta wa uzio na jengo la usimamizi lenye nafasi ya kutosha ya ofisi. Jumla ya miradi 14 imesajiliwa na inafanya shughuli za kuzalisha bidhaa za kuuza ndani na nje ya nchi. Miradi hiyo ni pamoja na kiwanda kikubwa cha nguo Tanzania,

kiwanda cha kuzalisha kadi za kielektroniki zikiwemo kadi za benki (Master and Visa Card), vocha za kukwangua, laini za simu, kiwanda cha kuzalisha kahawa, viwanda vya kusindika mazao yakiwemo ya ufuta, dengu, mbaazi, choroko na korosho, kiwanda cha kutengeneza vifungashio.

Eneo hili lenyewe lina miradi ya viwanda vilivyotoa ajira za moja kwa moja zaidi 4,761 kwa Watanzania wengine wasio na ajira za moja kwa moja 1,500, huku mauzo ya nje ya nchi kiasi cha Dola Milioni 70 yakifanyika kila mwaka.

**b. Mradi wa Bagamoyo SEZ**

Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone -BSEZ), ni mradi wa Taifa wa kielelezo (National Flagship Project) katika kutekeleza azma ya kufikia lengo la Tanzania kuwa na uchumi wa kati na endelevu ambao mhimili wake mkuu utakuwa ni viwanda kama sekta kiongozi.

Mradi huu unahusisha ujenzi wa bandari ya kisasa na ya kimataifa itakayotumika kama moja ya njia ya usafirishaji wa bidhaa za kimataifa. Mradi wa bandari utaunganishwa na mradi wa ujenzi wa eneo la viwanda ambalo litatoa fursa za kutengeneza bidhaa mbalimbali pamoja na kuongeza thamani za bidhaa kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje ya nchi.

Katika kipindi husika, Mamlaka kupitia Mtaalam Mshauri ABECC ya Chuo Kikuu Ardhi, imekamilisha kuhuisha upembuzi yakinifu (feasibility study) na mpango kabambe (Master Plan) katika eneo husika. Kwa sasa, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami (Asphalt Concrete) yenye urefu wa kilomita tatu katika eneo Bagamoyo SEZ lililoanza kujengwa viwanda lililopo Zinga chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura).

Mkandarasi alianza kazi rasmi Januari, 19, mwaka 2023. Hadi sasa Mkandarasi amekamilisha

kazi husika kwa asilimia sitini (60.9).

**c. Manyara SEZ**

Mradi huu ni kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata madini ikiwemo madini ya Tanzanite, kuchakata mazao ya kilimo na mifugo kwa sababu malighafi hizo zinapatikana kwa wingi katika Mkoa wa Manyara na Arusha. Hii inatokana na utajiri mkubwa wa aina mbalimbali za madini yaliyopo katika eneo hili ikiwemo Tanzanite ambayo haipatikani sehemu nyingine yoyote duniani. Eneo hilo lina ukubwa wa hekta 406 na lipo katika Kijiji cha Kandasikra likipakana katika Mji mdogo wa Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Katika kipindi husika, Mamlaka ya EPZA kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi (Consultant) ambaye ni Taasisi ya Bureau for Industrial Cooperation (BICO) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, imeendelea na utekelezaji wa kazi ya upembuzi yakinifu na kuandaa mpango kamambe wa eneo la Manyara SEZ ili kuliandaa kwa ajili ya uwekezaji. Hadi sasa Mshauri amekamilisha kazi hiyo kwa asilimia 90.

**d. Nala SEZ**

Eneo hili limepangwa kuendelezwa kwa ajili ya kuyaongezea thamani mazao ya kilimo, uwekezaji wa viwanda vya vifaa vya ujenzi, viwanda vya dawa, viwanda vidogo (light industry) na pia uwekezaji katika utoaji huduma za msingi.

Mazao yanayolengwa ni alizeti, zabibu nakKaranga. Eneo hili liko katika Mkoa wa Dodoma na lina ukubwa wa ekari 1,500.

Katika kipindi husika, Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ, imeshakamilisha na kulipa fidia kwa Jiji la Dodoma ili kuhamisha umiliki wa eneo hilo.

**e. Kwala SEZ**

Eneo la Kwala SEZ, ni eneo ambalo Mamlaka ya EPZ imekabidhwa ikiwa ni mbadala wa eneo la Kituo cha Ugavi na Biashara Kurasini baada ya uamuzi wa Serikali kupitia kikao kilichofanyika tarehe Aprili 2, mwaka 2022 kuhamisha umiliki wa eneo lote la Kurasini kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA).

Serikali ilielekeza EPZA ipewe eneo lenye ukubwa wa ekari 100 katika eneo la Bandari Kavu la Kwala na TPA igharimie ujenzi wa miundombinu ya msingi (barabara, umeme, mifumo ya maji safi na maji taka, njia za mawasiliano na ujenzi wa jengo la utawala). Hati ya eneo tayari imepatikana na Mamlaka imekamilisha hadidu za rejea ili kumpata mtaalam wa kuandaa michoro na gharama za miundombinu ya msingi na kuziwasilisha katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari.

**f. Ruvuma SEZ**

Eneo hili limepangwa kuendelezwa kwa ajili ya kuyaongezea thamani mazao ya kilimo hususani kutoka Mkoa wa Ruvuma na mikoa jirani. Eneo hili liko katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma na lina ukubwa wa hekta 2,033.

Aidha, wakati zoezi la uhakiki (disclosure) na ulipaji fidia wa awamu ya pili likiendelea, walijitokeza wananchi ambao walikuwa na nakala za fomu za uthamini wa uwandani, lakini majina na taarifa zao hazipo kwenye jedwali lililoidhinishwa mwaka 2009 na Mthamini wa Manispaa pia hakuwa na kumbukumbu za taarifa zao. Kwa sasa suala hisika lipo katika uchunguzi na malipo ya fidia yataendelea mara baada ya kukamilika kwa uchunguzi huo.

**g. Mradi wa maboresho ya mifumo ya utoaji wa huduma kwa wateja kwa kutumia TEHAMA**

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Septemba, 2023, Mamlaka kwan ufadhili wa TradeMark Africa (TMA), imeendelea na ujenzi mfumo wa TEHAMA wa utoaji huduma kwa pamoja kwa wawekezaji (EPZA Business Facilitation Portal).

Lengo la mfumo huu ni kuhakikisha Mamlaka inaboresha utoaji huduma kwa wawekezaji. Mfumo huu utasaidia Mamlaka kutoa huduma zake kwa ufanisi.

Mfumo upo kwenye hatua za mwisho za majaribio ya kuunganisha (integrate) mfumo wa malipo serikalini (Government Electronic Payment Gateway – GePG) na mfumo wa EPZA wa kielektroniki (EPZA BFP) ili kuwezesha malipo kwa kutoa ankara pepe.

Timu ya wataalam kutoka Wizara ya Fedha (GePG), EPZA na InfoWise Systems Ltd, inaendelea na majaribio ya mwisho kabla ya kuanza kutumika.

Aidha, Mamlaka ya EPZA imeendelea kutumia mfumo wa MUSE katika kufanya malipo yote ya Mamlaka ya EPZA.

**4. HITIMISHO**

Mamlaka ya EPZ, imejipanga kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha kuwa uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi unaendelea kukua na kuleta matokeo chanya katika uchumi sambamba na malengo ya Serikali ya kukuza uwekezaji na kujenga Tanzania ya viwanda.

Ili kufanisha azma hiyo, Mamlaka imepanga kuendelea kutekeleza miradi yake na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini, kusajili viwanda kutoka ndani na nje ya

nchi pamoja na kutoa huduma bora kwa wawekezaji wake kupitia dirisha la pamoja (One Stop Service Centre) ili kuhimili ushindani katika anga za uwekezaji kimataifa kwa manufaa ya nchi yetu.

Wawekezaji wanaoweza kuwekeza katika Uzalishaji wa Bidhaa za kuuza nje ya nchi walau asilimia 80 ya bidhaa na mtaji walau wa Sh. milioni 230 wanakaribishwa sana kujiunga na EPZA ili kupata elimu, vibali na usaidizi wa kitaalam.



# PONGEZI

**MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA UHURU MEDIA GROUP (UMG), TUNAKUPONGEZA KWA KUTIMIZA MIAKA MITATU MADARAKANI.**

**HAKIKA IMEKUWA NI YA KISHINDO NA KAZI INAONGEA.**

**TUNAKUOMBEA MAISHA MAREFU YENYE AFYA NA MAFANIKIO KAZINI. WATANZANIA TUPO PAMOJA NAWE NA TUTAKUUNGA MKONO SIKU ZOTE KWA MASLAHI YA TAIFA LETU. AHSANTE**

# Imebeba makubwa kwenye sekta ya elimu



> Katika kipindi kifupi cha miaka mitatu ya urais wake, Rais Samia amefanya makubwa akileta mabadiliko katika elimu ngazi zote kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu kwa kuwekeza ipasavyo, ujenzi wa majengo na miundombinu, ubadilishaji wa sera na mitaala, unoaji wa walimu, kuwasukuma wasichana kielimu na kadhalika na kadhalika.

**Na Hamisi Kibari**

WAZUNGU wana usemi kwamba, kama unadhani elimu ni ghali, jaribu ujinga! Moja ya maana za usemi huu ni kwamba, usipowekeza kwenye elimu, utabaki mbumbumbu mzungu wa reli.

Taifa lisipowekeza kwenye elimu litakosa wataalamu wa kuendesha nchi katika uchumi wa kisasa. Kutakuwa na shida kama si uhaba wa walimu, wahandisi, marubani, waandishi wa habari, wakulima wa kisasa, wahasibu, wauguzi na kadhalika na kadhalika.

Tusiende mbali, zipo taarifa kwamba kuna vituo vya afya nchi hii hii vimepelekewa vifaa tiba, mathalani mitambo ya radiolojia lakini haijaanza kuhudumia wananchi kutokana na uhaba wa wataalamu wa hiyo fani. Hiyo inatupa umuhimu makubwa wa nchi kusomesha vijana wake kadri inavyoweza.

Mwalimu Julius Nyerere alipata kusema kwamba ukitaka kumsaidia mtoto wa maskini, mpe elimu.

Ni kweli kabisa. Usipomsomesha mtoto wa maskini, basi unasababisha familia husika kubaki na mzunguko wa umaskini miaka nenda, miaka rudi. Dhana si lazima kwamba mtoto huyu wa maskini atapate ajira na kuikwamua familia yake kutoka katika umskini, bali matarajio ni kwamba atakuwa na maono mapana. Kama familia yake ilikuwa ya wakulima kwa ajili ya kujikimu, tunamtazamia aboreshe kiwe kilimo biashara.

Ukisoma makala haya mpaka mwisho, utagundua kwamba tunaye kiongozi wa nchi anayeyajua yote haya na mengine ambayo hayajachambuliwa katika utangulizi huu kuhusu umuhimu wa elimu.

Julai 26, 2023 aliposhiriki mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika kuhusu rasilimali watu, Rais Samia Suluhu Hassan alisema:

"Tupo tayari kuwekeza kwenye elimu na tumeanza na elimu ya awali ambapo elimu ya awali zamani ilikuwa ni kama sehemu wachimba madini (ambako ungeiona), lakini wakulima wanaweka tu vibanda ili watoto wao wasome pale lakini kama serikali tumejenga shule za kisasa kabisa ambazo watoto wale wanasoma."

Katika kipindi kifupi cha miaka mitatu ya urais wake, Rais Samia amefanya makubwa akileta mabadiliko katika elimu ngazi zote kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu kwa kuwekeza ipasavyo, ujenzi wa majengo na miundombinu, ubadilishaji wa sera na mitaala, unoaji wa walimu, kuwasukuma wasichana kielimu na kadhalika na kadhalika.

**PESA ZA UVIKO 19**

Mwishoni mwa 2021, Tanzania ilipata mkopo wa shilingi trilioni 1.3 uliotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ili kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya korona. Tanzania ikaja na mpango wa kuinua uchumi kwa kutumia fedha hizo.

Kwa kujua umuhimu wa kuwekeza katika elimu, sekta mojawapo iliyopata mgawo wa fedha hizo ni elimu. Na kwa sababu ilikuwa ni kipindi cha kuelekea mwisho wa mwaka sehemu kubwa ya fedha hizo ilitumika kujenga madarasa takribani 15,000.

>>>Inaendelea Uk. 29







> **Kwa upande wa kuongeza fursa za elimu bajeti ya fedha za mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka Sh bilioni 570 katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi kufikia bilioni 654 mwaka 2022/23.**

# Imebeba makubwa kwenye sekta ya elimu

>>>Inatoka Uk. 28

Ni kutokana na hali hiyo, wanafunzi 9,780 waliofanya mtihani wa darasa la saba mwaka 2021 wote waliofaulu la saba walianza kidato cha kwanza kitu ambacho kilikuwa hakijawahi kutokea katika nchi yetu kwa muda mrefu.

Serikali pia ilitenga Sh milioni 600 kwa ajili ya kujenga shule mpya na mpango ulikuwa kwamba hadi kufikia 2025 zitakuwa zimejengwa shule za sekondari za wasichana 26.

### MAGEUZI SERA YA ELIMU NA MITAALA

Rais Samia wakati wa kulihutubia Bunge, alisema serikali yake imedhamiria kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya mabadiliko ya mitaala iliyopo ili ijielekeze kwenye kutoa elimu na ujuzi kulingana na mahitaji ya soko kitaifa, kikanda na kimataifa.

Ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia kumeshuhudiwa maboresho makubwa katika sekta ya elimu na utekelezaji wa kazi kulingana azma yake ya kuhakikisha elimu inakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa kutoa wahitimu wenye ujuzi na stadi.

Bila kwenda kwenye maboresho ya sera, kwa mujibu wa mtaala mpya kutakuwa na mkondo wa masomo ya jumla kama ilivyo sasa na mkondo wa masomo ya amali. Mkondo wa Elimu ya Amali umegawanyika katika michepuo ya fani za kilimo na ufugaji, umakenika, sanaa bunifu, michezo, ufugaji wa nyuki, urembo, n.k.

Mbali na masomo hayo mwanafunzi pia atasoma masomo ya Hisabati, Elimu ya Biashara, Kingereza na Historia ya Tanzania pamoja na Maadili ili kupata stadi za msingi katika mawasiliano, stadi za maisha na uzalendo.

Somo la Ujasiriamali ambalo kwa sasa Wizara iko katika mchakato wa kufundisha walimu litakuwa linafundishwa kwa wanafunzi wa mikondo yote.

Wizara ya Elimu pia imefanya mapitio ya mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi pamoja na Elimu ya Juu katika kuhakikisha elimu inayotolewa ni bora na inawajengea wahitimu kuwa na ujuzi na maarifa yatakayowapatia stadi zitakazowawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi kitaifa na kimataifa.

### ELIMU YA JUU

Kwa upande wa elimu ya juu, Serikali imeendelea kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya juu wanasoma katika mazingira rafiki na wezeshi. Serikali ilitafuta na kupata mkopo wa Sh bilioni 972 wenye riba nafuu kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Lengo la hatua hiyo ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu pamoja na kuongeza kampasi hadi kufikia 14, hususani katika mikoa ambayo haina vyuo vikuu ikiwemo Kigoma, Ruvuma, Singida, Mwanza, Kagera, Tanga, Buyu Zanzibar, Tabora, Manyara, Simiyu, Shinyanga, Lindi, Rukwa na Katavi.

Mradi pia unahusisha ujenzi wa mabweni 34; vyumba vya mihadhara na madarasa 130; kumbi za mikutano ya kisayansi 23; maabara/karakana za kufundishia 108; miundombinu ya shambani na vituo atamizi 10 hatua ambayo itasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za kipaumbele za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu (STEM) kutoka wanafunzi 40, 0000 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 106,000 ifikapo mwaka 2026.

Pia mradi umehusisha uboreshaji wa mitaala ya programu za kipaumbele cha Taifa kwa kuhuisha na kuandaa mitaala mipya zaidi ya 290, kusomesha wahadhiri 387 na wahadhiri 3500 wanatarajiwa kupata mafunzo kwa vitendo viwandani ifikapo mwaka 2026.

### MIKOPO ELIMU YA JUU

Kwa upande wa kuongeza fursa za elimu bajeti ya fedha za mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka Sh bilioni 570 katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi kufikia bilioni 654 mwaka 2022/23 hivyo kufanya jumla ya wanufaika kuongezeka kutoka wanafunzi 177,892 mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 202,016, kwa mwaka 2022/23.

### MPANGO WA SAMIA SKOLASHIPU

Serikali pia imeanzisha mpango wa kusomesha wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa Kidato cha Sita katika masomo ya Sayansi ambayo ni moja ya kipaumbele cha Taifa kupitia Mpango wa Samia Skolashipu.

### UFUNDI STADI

Katika kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi, Serikali imefanya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vya wilaya 25 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko 19.

Serikali inaendelea kutenga mabilioni ya fedha katika kutekeleza azma ya kuwa na chuo cha VETA katika kila wilaya na katika kila mkoa kwa kujenga vyuo zaidi 64 kwa kuanza na Mkoa wa Songwe ambao hauna chuo katika ngazi hiyo.

Serikali pia imejenga chuo kipya cha kisasa cha Ufundi Dodoma chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 15,000 kwa mara moja.

### KUKUZA WABUNIFU

Katika sekta ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Serikali imekuwa ikiibua wabunifu ambapo hadi mwaka jana wabunifu 1,581 waliibuliwa ambapo kati yao 153 walitambuliwa na 27 kuendelezwa huku tisa kati yao wakifikia hatua ya kuziwezesha tafiti zao kuwa biashara sokoni.

Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yamekuwa yakipelekwa mpaka katika ngazi ya wilaya, lengo likiwa ni kuwapata wabunifu waliopo chini na kukuza ubunifu na teknolojia zinazozalishwa.

### ELIMU MAALUMU

Serikali kila mwaka inatenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kuboresha elimu maalumu ikiwa ni pamoja kununua vifaa mbalimbali kama viti mwendo, vitabu vya kutosheleza vya nukta nundu, maandishi makubwa pamoja na vifaa vya kusaidia usikivu.

### KURUDI SHULE

Moja ya jambo kubwa lililofanywa na uongozi wa Rais Samia ni kuwarudisha shuleni wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali.

Kimsingi, elimu ni pana na ina vikorokoro vingi lakini vyote hivyo vikiwemo ambavyo makala hii haijazijadili, vimeboreshwa katika uongozi wa Rais Samia.

# Mapinduzi ya Sanaa na Utamaduni katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia

**Na Valensi Mbaga**

SEKTA ya sanaa na utamaduni nchini Tanzania imekuwa na mchango mkubwa katika uchumi na utambulisho wa nchi.

Tangu enzi na enzi kumekuwa na mafanikio mbalimbali katika kukuza sanaa na utamaduni wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan sekta hii imekutana na mafanikio makubwa ambayo hayakuwahi kufikiwa kabla.

Sekta hii kwa sasa Imekuwa na ukuaji katika suala la pato , ubunifu, na wasanii wakigundua namna na njia tofauti za kujiendeleza huku wakipata hamasa na misaada mbali mbali kutoka kwa serikali.

Katika hatua mojawapo ya kukuza sanaa yetu Rais Samia Suluhu Hassan aliingia mkataba na muigizaji maarufu kutoka nchini marekani , Idris Elba ikiwa ni moja ya hatua ya kukuza uzalishaji bora wa sanaa itakayoendana na soko la dunia.

Lakini pia Wasanii wa Tanzania wamepata kutambulika katika jukwaa la kimataifa, kwa kushiriki katika maonyesho ya kimataifa na matamasha. Hili sio tu limeonyesha vipaji na ubunifu wa wasanii wa Tanzania bali pia limesaidia katika kukuza urithi wa utamaduni wa nchi.

Zaidi ya hayo, serikali na wadau wengine wamejitahidi kusaidia na kuwekeza katika sekta ya sanaa na utamaduni. Juhudi kama vile programu za ufadhili, hafla za kitamaduni, na ukuzaji wa miundombinu zimesaidia katika kukuza vipaji na kuhifadhi urithi wa kitamaduni wa Tanzania.

Mchango wa Rais Samia Suluhu Hassan ulienda mbali zaidi na wasanii wamekuwa wakipatiwa mikopo ya muda mrefu kwa ajili kuboreha kazi zao na kutengeneza mfumo wa kujitegemea.

Kupitia mfuko wwa utamaduni kumekuwa na fursa nyingi mpya zilizoletwa na Rais Samia ambapo wasani kutoka kada mbalimbali wamepewa mikopo pia kwa ajili ya kununulia vifaa, kufanya masoko na mengine mengi ili kuhakikisha wanajiogezea kipato na kufunga fursa kwa vijana wengine.

Mikopo hii yenye riba nafuu imewasaidia sana wasanii wote ambao kwa hali moja au nyingine wasingeweza kufikia malengo yao na wengine kupoteza vipaji vayo na kuishia mitini tu.

Lakini pia moja kati ya jambo kubwa na la umuhimu zaidi ni namna Rais Samia alivyofanya sanaa kuonekana kama kazi rasmi kwani kwa kipindi cha hivi karibuni ilionekana kama uhuni tu.

Kwa hatua hio Rais Samia Suluhu Hassani amerejesha heshima kwa sanaa ya Tanzania na kuirudisha katika hadhi yake kama ilivyokuwa toka zamani enzi zile za kupigania uhuru ambapo wasanii walikuwa mstari wa mbele kutengeneza mashairi ya kuiasa jamii kupambania uhuru wao.

> "Serikali na wadau wengine wamejitahidi kusaidia na kuwekeza katika sekta ya sanaa na utamaduni. Juhudi kama vile programu za ufadhili, hafla za kitamaduni, na ukuzaji wa miundombinu zimesaidia katika kukuza vipaji na kuhifadhi urithi wa kitamaduni wa Tanzania.



Sio hayo tu lakini pia bado serikali imeonekana kuwatumia wasanii katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kuelimisha jamii.

Na serikali chini ya Baraza la sanaa Tanzania (BASATA) wameboresha utaratibu wa maadili kwa wasanii na kuweza kulinda misingi bora ya tamadni zetu.

Elimu mbalimbali ikiwa ni pamoja na onyo kwa aliyekiuka sheria hizo zilizochukuliwa ili kudumisha umoja na mshkamano kwa wasanii wote pamoja na BASATA





# Kesi ya Prince Dube na usingizi mzito wa Azam

**Na Ibrahim Mkamba**

KUNA ukosoaji anaofanyiwa Prince Dube kwa asemayo akiwa katika kuagana na Azam FC. Tunamkosoa kwa kuvujisha siri. Siri zipi? Nani asiyejua Azam FC huzinufaisha Simba na Yanga kwa zamu kutegemea idadi ya mashabiki wengi ya Simba na Yanga waliopo kwenye uongozi wa klabu hiyo?

Mashabiki wa Simba walipokamata uongozi wa klabu hiyo, Simba ilikuwa ikiifunga kirahisi Azam FC tena mfululizo. 4-2, 2-0 na kadhalika. Yanga ilikuwa ikiteseka mno kwa Azam FC.

Sasa ni zamu ya Yanga kucheka kwa kutokana na uongozi wa sasa wa Azam FC.

Simba wako taabuni. Kuna siri gani hapo? Prince Dube amekuwa jasiri kusema kwani wengine hawasemi. Kasema viongozi wa Azam FC huwa na timu zao wazishabikiazo zinapopambana na Azam FC. Ni jasiri tu wa kuliweka hilo hadharani. Wengine tunanong'ona tu.

Viongozi wa Azam FC na klabu nyingine wajitafakari. Wafanye kazi kwa maslahi ya taasisi zao.

Marehemu George Mpondela akiwa anaifanyia kazi Pamba FC ya Mwanza ile ya moto mkali ya TP Lindanda aliwahi kusema "linapokuja suala la timu yangu ya kazi ya Pamba FC dhidi ya timu yangu ya Yanga ninayoishabikia, nahakikisha napambania maslahi ya timu yangu ya kazi ya Pamba hata nikiumia Yanga kukwama.

Nikizidiwa na ushabiki nitaamua kwenda huko huko Yanga kufanya kazi nao lakini kamwe sitaisaliti Pamba nikiwa ndani ya Pamba ya Mwanza."

Ni kauli ambayo viongozi wa soka wa klabu nyingine wanapaswa kuishi nayo.

Jingine lililonifanya nimuone Prince Dube kuwa mtu jasiri sana ni kauli yake ya kusema Azam FC haina malengo makubwa.

Akabainisha kwamba msimu wanauanza kwa moto kisha moto huo kuzimika.Hapo kuna siri gani? Labda angebanwa aeleze ni nani wa kwenda na ukali wa moto mpaka mwisho kama si wao wachezaji na yeye akiwemo?

Lakini ukiitafakari kauli yake hiyo, utaona kweli uongozi wa Azam FC una maajabu yake.

Azam FC si kama Tabora United au Mashujaa ya Kigoma. Wamecheza ligi kuu tangu 2008.

Wamebeba ubingwa wa ligi kuu si mara moja, Shirikisho mara kadhaa, ngao ya jamii mara kadhaa.

Wameiwakilisha nchi mashindano ya Afrika mara kadhaa na linalosisimua zaidi, wao, nje ya Simba na Yanga, ndiyo timu pekee ya Tanzania iliyobeba kombe la Kagame la ubingwa wa Afrika Mashariki na ya kati.

Pamoja na wasifu wote huo mkubwa, leo viongozi wa Azam FC wanaibuka ligi kuu ikifikia katikati na kusema kwamba eti msimu huu na miwili ijayo hawana lengo la kupambania ubingwa bali kwa miaka mitatu wanatengeneza timu ya kupambania ubingwa. Kwa misimu mitatu!

Hii ni kauli ya ajabu mno kwa klabu yenye timu iliyokwishafanya makubwa yaliyoelezwa.

Wangesema hivyo Mashujaa au Tabora United ingeeleweka. Hata timu nyingine, nje ya Tabora United na Mashujaa, ambazo hazijafikia maendeleo ya Azam FC kwa muda mrefu, nazo zinaweza kuhalalishwa kueleza hivyo lakini si Azam FC.




Hao wachezaji wakubwa wa ndani na nje wa Azam FC wa nini sasa kama lengo si kugombea ubingwa?

Pigia mstari neno 'kugombea' na litofautishe na neno 'kubeba'. Hata kugombea ubingwa, Azam FC haigombei? Ipo ligi kuu kumsaidia nani abebe ubingwa na nani asishuke daraja?

Dube anapolalamika kwamba amechoka kuchezea timu ya klabu yenye malengo madogo, kuna tunaomlaumu.

Dube ni jasiri. Hivi tulitaka tunapomuuliza sababu za kutaka kuondoka Azam FC asiseme chochote? Katoa sababu hizo zake, tunamlaumu.

Hizo ni sababu zake na kwa nini tunataka tumlazimishe atoe sababu tuzitakazo?

Dube ni jasiri kuuamsha uongozi wa Azam FC kuwa na ndoto kubwa kutokana na ukubwa wa klabu, makubwa iliyokwishayafanya na ukubwa wa wachezaji wao.


Wasipoamka, wengi kutoka Azam FC watamfuata jasiri Prince Dube.

**Ibrahim Mkamba ni Mwandishi wa Habari na Wakili wa Kujitegemea.**

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumanne Machi 19-26, 2024 |



# Miaka mitatu ya Rais Dk. Samia katika michezo

Na Valensi Mbaga

IKIWA imetimia miaka mitatu toka historia iandikwe katika nchi ya Tanzania ambapo mara ya kwanza Rais Mwanamke aliingia madarakani huku mengi yaliyoshindikana yakipatiwa majibu katika sekta ya michezo.

Ni ukweli usiofichika kuwa pamoja na mafanikio yote yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali za michezo ni matokeo ya moja kwa moja ya mkono wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mafanikio makubwa katika miaka hii mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan katika michezo yanaonekana katika pande zote za kimchezo ikiwemo mpira wa miguu katika ngazi ya vilabu na taifa kwa ujumla,kuogelea, golf, mpira wa wanawake, mpira wa nyavu, mpira wa kikapu pamoja na uboreshaji wa miundombinu stahiki kwa ajili ya kuendeleza michezo.

### Kushiriki na kuandaa mashindano ya kimataifa

Baada ya miaka kadhaa kupita hatimae kwa mara nyingine tena tukapata nafasi ya kushuhudia timu zetu za Taifa zikishiriki mashindano makubwa na kuonyesha ushindani mkubwa.

Taifa stars ilishiriki michuano ya AFCON 2023 kule nchini Ivory Coast mwaka huu na kufanikiwa kuonyesha ubora na kukua kwa soka letu.

Twiga stars wao tayari wameshafanikiwa kujinyakulia tiketi ya kushiriki WAFCON itakayofanyika mapema mwezi june huko nchini Morrocco pamoja na kushiriki olympiki.

Mwaka 2027 michuano ya Afcon inatarajiwa kufanyika katika ukanda wa Afrika mashariki na Tanzania ikichaguliwa kuwa moja kati ya nchi tatu zitakazokuwa wenyeji wa michuano hiyo ikishirikiana na Uganda pamoja na Kenya.

Mazao yote haya yanaletwa na uwekezaji bora na uliotukuka wa Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya michezo. Na uboreshwaji wa miundombinu kama viwanja vya kisasa na vinavyofikika vema kutokana na miundombinu salama ya barabara.

### Uwekezaji na mafaniko katika nyanja nyingine za michezo

Pamoja na mafanikio hayo lakini uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuongeza ushiriki wa serikali katika kusapoti michezo ya aina yote kumepelekea Tanzania kukua zaidi kimichezo.

Idadi ya timu zinazoshiriki mashindano ya kimataifa imeongezeka kutokana na serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa ( BMT) kuwezesha timu na wanamichezo kusafiri bila wasi wasi kwa kusaidiwa nauli. Hatua hiyo ilipelekea timu ya kuogelea kufanikiwa kuiwakilisha vyema Tanzania na kurudi na medali za dhahabu katka mashindano ya Afrka yaliyofanyika Rwanda.

Timu ya golf nayo haikuwa nyuma kwani walifanikiwa kufanya vizuri katika michuano ya Afrika na kushika nafasi ya tatu.

### Hamasa katika michezo

Katika historia ya soka la Tanzania,jina la Rais Samia litaimbwa milele kwani katika kipindi cha miaka hii mitatu amekuwa na msukumo mkubwa wa kuwapa motisha wanamichezo wote nchini kwa kuwapongeza wanapofanya vizuri na kuwafariji wanapofanya vibaya.


Kwenye upande wa mpira wa miguu Rais Samia Suluhu Hassan alianzisha hamasa ya kununua goli katika michezo muhimu iliyoweka heshima na historia katika nchi yetu.

Rais aliandaa utaratibu wa kununua magoli (kapu la mama) kwa timu zilizokuwa zikiwakilisha bendera ya Tanzania katika michuano mikubwa kwa ngazi za vilabu pamoja na timu za taifa.

Twiga stars pamoja na Taifa stars kwa pamoja zikinufaika na kapu la mama lililowapa motisha kwa kitita cha shillingi Milioni 200 kwa kila mmoja ili kuwapa nguvu ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michezo.

Kwa ngazi ya vilabu kapu la mama lilianza kutoa motisha katika michezo ya klabu bingwa Afrika na kombe la shirikisho msimu uliopita ambapo kila goli Rais Samia alitoa sh. Millioni 10. ambapo timu mbili yani Simba SC pamoja na Yanga SC zikikutana na neema hii kwani ndio waliokuwa wawakilishi wa Tanzania katika michuano hiyo.

Kwa motisha hiyo ilipelekea historia nyingine kubwa kuandikwa kwani klabu ya Yanga SC lifanikiwa kucheza fainali ya kombe la shirikisho na kushika nafasi ya pili na kuona hio haitoshi Rais Samia aliwaalika mashujaa hao katika viwanja vya ikulu ili kupata mlo wa jioni ikiwa ni sehemu ya pongezi kwao pamoja na kuwahusia kupambana zaidi kwa ajilin ya heshima ya nchi.





> Katika kipindi kifupi tu cha miaka mitatu ya Rais Samia tumeshuhudia matukio makubwa ya kihistoria.



### Kukua kwa Miundombinu rafiki na yenye ubora

Katika kipindi kifupi tu cha miaka mitatu ya Rais Samia tumeshuhudia matukio makubwa ya kihistoria katika michezo hasa eneo la miundombinu rafiki na ya kisasa.

Kwa mara ya kwanza mashindano makubwa kabisa ya soka kwa ngazi ya klabu ( African Super League) yalizinduliwa hapa nchini katika dimba la Benjamini Mkapa huku timu ya Simba SC ikiwakilisha Tanzania katika michuano hiyo ambayo pia ilihudhuriwa na watu mashuhuri kutoka katika kona mbalimbali za ulimwengu. Akiwemo Rais wa FIFA Gianni Infantino na kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger.

Sio hayo tu lakini pia timu mbalimbali kutoka mataifa mengine kama Sudan, Kongo ziliomba kuweka makazi Tanzania kwa ajili ya kutumia viwanja kwa mechi zao za kimataifa.

Hii inadhihirisha ubora wa miundombinu yetu lakini pia amani ambayo imetawala na yoote kwa pamoja utawala bora kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

### Historia mpya ikaandikwa

Ukurasa mwingine ulianza kuandikwa chini ya Rais Samia baada ya Tanzania kupeleka timu mbili katika michuano ya klabu bingwa Afrika.

Mafanikio yakazidi kuonekana chini ya uongozi wa Rais Samia na alizidi kuzitia moyo na kuwapa pongezi wawakilishi hao katika kila hatua.

Hatimae Yanga SC pamoja na Simba SC zikafanikiwa kutinga hatua ya robo fainali kwa pamoja. Na kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Tanzania timu mbili kufika hatua hiyo kwa pamoja.

Timu mbili kwenye hatua ya robo fainali ni jambo kubwa sana la kujivunia kwa mpira wetu. Na ni mafanikio ambayo hakuna nchi imefikia kwa msimu huu kwani Tanzania ndio nchi pekee yenye timu mbili katika hatua ya robo fainali na yote yameletwa kutokana na uwekezaji wa hali ya juu ndani ya miaka hii mitatu ya Rais Samia .

Uwepo wa Rais Samia Suluhu Hassan ni neema katika sekta ya michezo na maendeleo ya nchi kwani imefungua uchumi katika sekta nyingine mbalimbali ambazo zilikuwa zimedorora hasa sekta ya hoteli na utalii.

Lakini pia kipato na uchumi wa watanzania vinazidi kuongezeka zaidi kupitia michezo kwani kuja kwa wageni kutoka sehemu mbali mbali inachangia sana katika kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Ni michezo iliyoipaisha na kuitangaza Tanzania mbali zaidi lakini yote haya ni juhudi na uadilifu wa dhati kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassani katika kipindi kifupi tu cha miaka mitatuna tutazamie makubwa zaidi kutoka kwake katika kpindi kilichobaki.